
MEI MMXXV - TOLEO LA XLIII

# NGURUMO
## ya Mwandishi



NGUGI WA THIONG'O
1938 - 2025

# 'MBUYU' WA FASIHI YA AFRIKA UMEANGUKA

**HABARI KUU:**

**TAFF Yalitambua Ngurumo ya Mwandishi, yamheshimisha Richard Mwambe**

## YALIYOMO

**TAHARIRI— Uk 02**
'MBUYU' WA FASIHI YA AFRIKA UMEANGUKA

**MWANDISHI WETU— Uk 03**
Lilian Mwita

**NEW IN TOWN: Uk 04**
KOSA LANGU, ENZI ZA UHAI WANGU

**PITIO LA VITABU— Uk 05**
KILIO CHETU '2'

**SAIKOLOJIA: Uk 06— 07**
NGUVU YA KUPAMBANA NA NYAKATI NGUMU

**MAKALA: Uk 08 - 09**
HUYU NI NGUGI WA THIONG'O

**KUTOKA KWA FANANI: Uk 10**
SALUM MAKAMBA ATUFUNZA

**Sako kwa Bako – Uk 11**
CLEMENTINA 'SE'MBEDULE

**RIWAYA: Uk 12—13**
MSALITI '4'

**RIWAYA: Uk 14—15**
Najutia Kuwa Na Wewe '3'

**YA KALE NI DHAHABU: Uk 16**
Alibaba na Wezi 40 '19'

**HABARI MOTO: Uk 17**
TAMASHA LA FASIHI YA KISWAHILI 'TAFF' LAFANA

**SHUBAKA LA VITABU: Uk 18**
HISTORIA YA VITABU 'Kitabu cha Watibeti''

**KITABU NILICHOSOMA: Uk 19**
SHOW YOUR WORK

**MATANGAZO: Uk 20**

**MALENGA WA KILEO: Uk 21**
BURIANI NGUGI WETU

**HABARI PICHA: Uk 22**
TAMASHA LA TAFF

**KUTOKA MAKTABA: Uk 23**
Maisha ni Mapambano '9'

**ELIMU JAMII: Uk 24**
SAFARI YA MALEZI—TONE LA LEO, UA LA KESHO

**MATUKIO: Uk 25**
Tumetunukiwa Tuzo ya Heshima

**HADITHI: Uk 26 - 27**
Happy New Year '6'

**HADITHI: Uk 28 - 29**
NGUVU YA KIAPO '01'

## TAHARIRI:
## 'MBUYU' WA FASIHI YA AFRIKA UMEANGUKA

Amani iwe kwenu nyote,

Toleo letu la 43 laja na huzuni na furaha kwa wakati mmoja. Tusemeje? 'Yote ya Mungu!'

Mwezi Mei umakuja na mazito katika fasihi yetu, Taasisi ya Mfuko wa Fasihi Tanzania ulikuwa na tamasha kubwa lililofana sana. Tamasha lililokusanya wapenzi na wanafasihi.

Lakini tukiwa tamashani siku ya kwanza tukapokea taarifa ya kifo cha nguli wa fasihi Afrika, Ngugi wa Thiong'o. hakuna asiyemjua mshititi huyu aliyejua kucheza na lugha asili katika kufuma visa vya kusisimua.

Naamini kutoka kwake kuna machipukizi mengi ya uandishi. Tumtakie buriani, maana wanazuoni wanasema '*mwandishi hafi maana huishi katika maandiko yake'*.

Basi, na tuungane tena katika toleo hili la 43, na jambo jema tu ni kuwa tumepokea tuzo ya heshima kupitia maandiko haya ikiwamo Ngurumo ya Mwandishi.

Lakini pia mwezi huu wa Mei tumeshuhudia maandiko mapya mengi, vitabu vikichapwa na kuingizwa sokoni. Hakika *washika kalamu* mmeamua, sisi wasomaji ni nani tupinge? Sisi hatupo bila ninyi na ninyi hampo bila sisi. Pikeni pikeni pikeni, walaji tu hapa tumekwishaandaa matumbo kuyajaza kwa maandiko na visa vipya.

Basi twende pamoja, kurasa kwa kurasa tukisoma na kuchambua.

Asante sana!
Wakatabahu!

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**WASILIANA NASI**
**0766 974 865 AU 0627160016**
**WhatsApp: +255 766974865**

# MWANDISHI WETU:
## LILIAN JOSEPH MWITA



**Katika safu yetu hii adhimu, twamleta kwako Mwandishi, Mwalimu na Fundi mitindo. Yeye alijinyakulia moja ya nafasi kumi na moja za ushindi wa hadithi fupi katika shindano lililoandaliwa na Tanzania Fasihi Fund (TAFF).**

**Haya, nisiwe msemaji sana, huyu hapa mwenyewe kutoka kuleee 'Kanda Maalum' karibu...**

Naitwa Lilian Joseph Mwita, nimezaliwa mkoani Iringa ila ni mwenyeji wa mkoa wa Mara Serengeti. Kitaaluma nimesoma shule za *kishua* kwa sababu wazazi wetu wasio wa *kishua* walichagua urithi watakaotuachia kuwa ni elimu na sina deni nao katika hili. Nimesoma Shule ya Msingi St. Benedict, Njombe.

Shule hii ilinifanya nikijue Kiingereza kwenye vipengele vyote vya *English language.* Nikiwa hapo nilisoma *composition, comprehension, grammar, structure* na *literature. Imagine* kuchambua *"Things Fall Apart"* nikiwa darasa la tano! Hapa ndipo uandishi ulianza moyoni mwangu ili nipate *marks* nyingi kwenye *composition* maana *structure* na *grammar* ilikuwa mtiti.

St. Francis Girls, Mbeya, hapa sasa kuna elimu ya kupata A na kuna somo la ushonaji, upishi na sayansi kimu yaani ukitoka unakuwa mama bora mshonaji mzuri na mpishi bora ukiwa na *division one* kama nyongeza. Hapa niliamua kuchagua ushonaji ndipo msingi wa 'Afrohome Bags and Tailoring' ulipojengwa na kuundwa vyema.

Marian girls Bagamoyo hapa katika kitovu cha kanisa katoliki na uinjilishaji Afrika Mashariki,hapa ndipo niliposoma Fizikia,Kemia na Baiolojia kwa ndoto za kuwa mwalimu wa madaktari.japo moyoni bado nikiwa na shauku ya kuandika na kunikuta najadili vitabu na watu wa lugha ilikuwa kawaida sana.

Shahada ya ualimu niliipata Chuo Kikuu cha St. Joseph Tanzania jijini Dar es salaam.

Hapa sasa safari yangu ya ualimu ilianza rasmi na sintoacha kufundisha maana nimeitwa kufundisha. Na sasa nimeanzisha *Afrohome Open School* kwa sasa tuna elimu ya awali na masomo ya ziada kwa sekondari na ushonaji.

Nilisema uandishi ni kitu kilikuwa moyoni toka shule ya msingi. Niliandika hadithi za mapenzi ya ki-shuleshule na kumpa mtu atembeze watu wasome na aseme ni yake. Furaha yangu ilikuwa nikisikia wanasimuliana. Nikiwa kazini nikakutana na ndugu mmoja *facebook* akaomba nimuandikie hadithi na nimuuzie. Nikaandika hadithi tatu na kuziuza. Kwa sasa hayupo duniani kifo kilimchagua, na kabla hajaondoka aliniambia kuwa *'sasa wakati wa kuandika kwa jina lako'* ijapokuwa moyo bado ulihofia na zawadi ya kumuenzi ni kutoa hadithi, maana alifariki hadhira ikiwa hawajaiona kazi hiyo. 2023 nilianza kuiandika japo bado haijakamilika maana ni ya kweli hivyo kabla sijaleta madhara kwenye maisha ya wengine, naeendelea kuumba.

Napenda sana mashairi na nimeandika baadhi kwenye ukuta wangu mtandaoni. Tangazo la shindano za hadithi fupi la TAFF lilinijia likiwa linaelekea ukingoni nikaamua kabla sijatoa kitabu changu wacha nishiriki shindano nione nasomeka kweli! Mara *paap*! Nikaona niko katika kumi na moja, bora. Kumbe naeleweka. Sasa ujasiri na ari ya uandishi vimeamka upya japo ndani yangu sitaacha kusimulia maana kama kuna kitu nakipenda kwangu ni hii sauti yangu. Ushindi wangu TAFF ni ngazi yangu kuja katika ulimwengu wa uandishi nikiwa si kivuli tena.

Kama mwandishi kivuli kuna vitabu vitatu vilichapwa na sasa nakuja kama mwandishi na kitabu cha FANIKIO ARDHINI na vingine viko jikoni vitakujia sokoni hivi punde. Je; wewe unapenda kuwa mwandishi? Kama jibu ni ndio anza sasa kuandika chagua uwanda unaoujua vyema tuletee usife na mawazo yako kichwani tuandikie na anza ulipo ata ukutani kwako mtandaoni andika andika andika usiache. ***L.M***

# NEW IN TOWN :
## KOSA LANGU, ENZI ZA UHAI WANGU

**KOSA LANGU**
**Vennita Mwita**




Paul aliuelewa vyema msemo wa wahenga wa nani kama mama. Aliuishi msemo huo kwa raha na buraha. Aliuishi kitajiri katikati ya lindi la umasikini. Hakupungukiwa chochote wala hakuhitaji ziada yoyote. Mama yake alimtosha.

Siku moja, dunia ikamfunza kikatili kuwa hakuna marefu yasiyo na ncha. Paul akamzika mama yake akingali mtoto mwenye kuhitaji kuchungwa, tena almanusura ya kuzikwa naye. Safari yake ya kuwajua walimwengu ikaanzia hapo.
Ndugu aliowatafuta walimkimbia na aliowakimbia ndiyo waliomtafuta. Siri nyingi zilizofichika zikaanza kuchomoza taratibu. Ikawa patashanika nguo kuchanika.

Riwaya ya Kosa Langu imebeba visa na mikasa ya kusikitisha, mafunzo na makumbusho juu ya mzunguko wa maisha.....

Kitabu hiki kinaanza kupatikana kwenye maduka yafuatayo kwa bei ya Tsh 20,000 tu!

**DAR ES SALAAM**
1) Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni Block 41 (0655 428085)
2) Posta Mpya, karibu na sanamu ya askari (0755 454152)
3) Elite Bookshops — Quality Center, Palm Village, Tangibovu

**DODOMA**
APE Bookshops, Shopper's Plaza (0745 199 860)
7) APE Moshi 0768 954365
8) APE UDSM 0658 780015
9) Elite - Shoppers Mikocheni 0743 952935
Kwa mikoa mingine tunaweza kumfikishia msomaji mpaka mkoa aliopo. Wasiliana moja kwa moja na:
Duka la KONA ya riwaya - 0655428085
Wahi mapema nakala yako, uunge mkono jitihada zetu za kuhuisha fasihi andishi ya kiswahili Tanzania.
Jipatie cha kwako kwa Tsh. 20,000…
Tuwasiliane, vipo kwa ajili yetu.. nicheki inbox au kwa simu.


**ENZI ZA UHAI WANGU**
**Issa Ramadhan**

Hili lilikuwa ni kosa kubwa sana ambapo lilipelekea baba yake kumuhamisha Shamsa na kumpeleka nchini Afrika Kusini kwenye shule ya wasichana Monko.

Lakini Isivyokuwa bahati kwake Shamsa alipofika nchini Afrika Kusini akaingia kwenye Kasheshe kubwa iliyopelekea mkasa huu usipoe..

Kitabu kinapatikana kwa shilingi elfu 15 utakipata kitabu cha kwanza na cha pili...

Tuwasiliane 0760458050



# KILIO CHETU—2



**TAMTHILIYA:** KILIO CHETU
**MWANDISHI:** MEDICAL AID FOUNDATION

**MCHAPISHAJI:** TANZANIA PUBLISHING HOUSE

**MWAKA:** 1995

**JINA LA MHAKIKI:** Mwalimu Daud Makoba

Inaendelea sehemu ya pili...

**WAHUSIKA**

JOTI

- Mhusika mkuu
- Hana elimu ya jinsia na mahusiano
- Anajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na wasichana wengi. Wengine wakiwa wakubwa kuliko yeye.
- Mwisho anakufa kwa UKIMWI

SUZI

- Mhusika mkuu
- Msichana mdogo anayesoma shule ya msingi
- Hana elimu ya jinsia na mahusiano
- Anajiingiza katika mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi mwenzake Joti, pia anaambukizwa UKIMWI na kupata mimba.

ANNA

- Msichana mwenye elimu ya jinsia na mahusiano
- Anakataa vishawishi vya wanaume kwa sababu anajitambua kwa kuwa ana elimu ya jinsia

MAMA SUZI

- Anashikilia mila na tamaduni za zamani
- Haungi mkono kuwapatia watoto elimu ya jinsia na mahusiano, anaamini kufanya hivyo ni kuwaharibu watoto

MJOMBA

- Mwanaume mtu mzima
- Anaunga mkono wazazi kuwapatia watoto wao elimu ya jinsia na mahusiano.

**MANDHARI**
Mandhari ya mjini yametumiwa na mwandishi. Pia kunayo mandhari ya; nyumbani, kijiweni, barabarani, n.k

**MATUMIZI YA LUGHA**
Tamathali za semi

i. Tashibiha. "*Wakapukutika kama majani ya kiangazi.*" Uk 1

ii. Sitiari. *"We mbwa mweusi."* Uk 10

iii. Takriri. *"vikawazoa, vikawazoa… vikawazoa."* Uk 3

iv. Tanakali sauti. *"pwi, pwi, pwi,"* uk 18

v. Tafsida. "*Kafa kwa kukanyaga nyaya.*" Uk 4

vi. Mubaalagha. "*mtu si mtu, kizuka si kizuka*" uk 4

2. Misemo, nahau na methali
i. Msemo. "*Wembamba wa reli treni inapita.*" Uk 7

ii. Msemo. *"Kukimbilia suti na nepi hujavaa."* Uk 28

iii. Methali. *"umeula wa chuya."* Uk 29

iv. Methali. *"shukrani ya Punda ni mateke"* uk 19

v. Nahau. "*nimekuvulia kofia*" uk 6




3. Picha na taswira
*"Dubwana"* –ugonjwa wa UKIMWI;
*"Nguru"* – aina ya Samaki wabaya–amefananishwa na mtu mbaya;

*Itaendelea toleo lijalo!*

SOMA VITABU
- Kwa afya ya ubongo wako
- Kwa kujiongezea maarifa
- Kwa burudani

USISITE
- Kumsimulia mwingine hadithi uliyosoma
- Kumfundisha mwingine yale uliyojifunza
- Kumshauri mwingine kitabu cha kusoma

NI VIZURI
- Kutembelea maktaba
- Maduka ya vitabu
- Kupiga stori na waandishi



**NGUVU YA KUPAMBANA NA NYAKATI NGUMU**

Habari yako mpendwa rafiki yangu, pasi na shaka kuwa wewe ni mzima wa afya ya mwili na akili. Ikiwa kuna changamoto yoyote inayokukabili nikusihi kutokujikatia tamaa katika changamoto hiyo. Kama tujuavyo hakuna mtu apendae matatizo na ikiwa yameshakukumba basi usiache kuomba dua kwa Imani yako, kuwa na subira ili Mungu afanye vile atakavyo.

Katika toleo hili nimeona niongee na wewe kuhusiana na nyakati ngumu. Nyakati ngumu ni nini?

Nyakati ngumu ni zile ambazo hutokea katika mfumo wa maisha ya kila siku ambazo huleta mtafaruku/ mfadhaiko wa fikra ndani ya akili ya mtu husika. Nyakati hizo ngumu husababishwa na matokeo ya mambo fulani yanayotokea na kuzalisha ugumu katika akili ya mtu husika.

**Maeneo yanayoweza kuleta nyakati ngumu**

Yapo maeneo au mambo mengi ambayo yanaweza kuleta nyakati ngumu katika maisha ya kila siku. Mfano.. Kazini, kwenye mahusiano, kwenye ndoa, kwenye hatua za ukuaji na kwenye mchakato wa malezi.

Maeneo hayo au katika mambo hayo ndipo mwanadamu anaweza kukumbana na maudhi yatakayompelekea kupitia wakati/nyakati ngumu. Ni upepo tu ambao huweza kutokea hata mtu akapata wakati mgumu ama pia mtu anaweza kusababishiwa nyakati ngumu kutokana na wale aliowaamini au wale wamzungukao au wakati mwingine mtu akajisababishia yeye mwenyewe katika kupitia wakati mgumu.

Unapopitia wakati mgumu katika jambo lolote ni wazi kuwa utahisi kuchanganyikiwa kiakili kwa yale mambo yanayotokea katika maisha yako ya kila siku. Yawezekana unapitia wakati mgumu katika kazi zako, katika maisha yako kwa ujumla, katika ndoa, mahusiano, malezi ya familia yako na sehemu zingine zozote.

USIKATE TAMAA! Usikate tamaa wala usivunjike moyo na kuruhusu kuelemewa na jaribu au tatizo lolote lile. Huo ni upepo tu na utapita kama upepo mwingine unavyopita.

Uwapo kwenye wakati mgumu,kisaikolojia ubongo wako huwa na nguvu kubwa sana ya kuzalisha uimara katika kupambana na mtihani au jambo lolote. Kumbe tunaweza kusema, uwapo kwenye changamoto yoyote ndio wakati ambao kwa mtu anaejitambua anakua imara sana kiakili. Sasa ule uimara wa wakati wa jambo/mambo magumu ndio tunaita "nguvu ya kupambana kwenye nyakati ngumu".Uimara hutokea kwa yule alie tayari kujitambua na kutambua aishije kwenye nyakati tofauti tofauti zimtokeazo katika maisha yake.

**Nguvu ya kupambana na nyakati ngumu**

Kila binadamu amepewa uwezo binafsi katika kupambana na maumivu yamkumbayo pale akutanapo na nyakati ngumu. Wengi hutumia njia mbalimbali katika kukabiliana na maumivu katika nyakati husika. Ipo nguvu ya ndani ya kila mwanadamu ambapo akiiamsha nguvu hiyo huamka na kumsaidia katika jambo husika.

Tuone mambo machache yanayoweza kusaidia katika kupambana na nyakati husika.

**A} VUMBUA UTULIVU WAKO**

Kila binadamu ana kile kitu ambacho akikifanya yeye binafsi anapata utulivu wa nafsi yake. Wapo watu ambao wakutanapo na wakati mgumu utulivu wao

huletwa kwa kuzungumza na ampendae, mwingine akifanya mazoezi anatulia, mwingine akisikiliza muziki anatulia na huku mwingine yeye akikaa mahali penye ukimya anapata utulivu. Mwingine akiwa kwenye wakati mgumu akavuta manukato mazuri anatulia. Ni vyema kuvumbua utulivu wako ili ukutanapo na wakati mgumu utulie na kujituliza.

**B} ZUNGUMZISHA NAFSI YAKO**

Ni katika wakati huo mgumu ambapo nafsi yako inakusikiliza sana wewe, uwapo katika wakati /nyakati ngumu zungumzisha/zungumza na nafsi yako, ieleze kile unataka, itulize nafsi yako.

**C} JITIE NGUVU**

Mfariji wa kweli ni wewe mwenyewe, mtiaji nguvu wa kweli ni wewe mwenyewe. Katika nyakati ngumu jitie nguvu, jipe uimara, uwe nguvu yako katika nyakati zako ngumu.

**D} MALIZA KICHWANI**

Ikiwa nyakati ngumu zimekutokea bila taarifa [ *ipo nguvu ndani yako ya kuzijua nyakati zitakazokutokea mbeleni, hiyo tutazungumza wakati mwingine panapo majaaliwa yake Mungu muumba na muumbuaji* ], basi maliza wakati huo kichwani mwako. Ndio! Wewe ndiye mwamuzi wa nyakati hizo zidumu katika kichwa na maisha yako. Maliza kila kitu kichwani mwako, chora ushindi wa nyakati husika kichwani mwako.
WEWE NI MSHINDI!

**VITABU VINAPATIKANA**

- JITIBIE KISAIKOLOJIA…TSH. 12,000
- SAIKOLOJIA YA MAHUSIANO NA NDOA … TSH. 10,000

**WASILIANA NAMI**
Simu: +255763013206
ILI KUPATA COPY YAKO.

NIWAPONGEZE UONGOZI WA JARIDA HILI, LA NGURUMO YA MWANDISHI KWA KUTUNUKIWA TUZO YA HESHIMA KUTOKA KATIKA TAASISI YA TAFF{TANZANIA FASIHI FUND}.
TUZO ZILIZOTOLEWA MSIMU WA TATU WA TAMASHA, 28 & 29/05/2025. TAMASHA LILILOKUA NA KAULI MBIU "RUDISHA KITABU NYUMBANI, KUSOMA SIACHI NG'O.

HONGERENI SANA, HAKIKA MNASTAHILI. ASANTE.

Madame NEEMA MGAO,

+255763013206,
DODOMA,
TANZANIA.

**KITABU MAISHA**

**DONDOO YA KWANZA - JUNE '25**

Anayesoma kitabu kamwe hawezi kuwa sawa na asiyesoma kitabu. Kitabu ni kikombozi cha fikra, kina uwezo wa kukuweka huru katika kila nyanja kama utakipa nafasi.

Kusoma ni *hobbie* lakini kila mtu anatakiwa kusoma ili kuwa huru. Maarifa ya kujikomboa yamefichwa kwenye kurasa za kitabu.

Wabisha?

Soma kitabu, kisha andika uliyojifunza. Na yale ambayo unaona ni mema kwako basi yabadili kutoka maandishi kuwa maisha Yako. Hii ndiyo maana nzima ya "KITABU MAISHA"

*Hekima ya Amata Ga Imba*



# 'MBUYU' WA FASIHI YA AFRIKA UMEANGUKA

"Fasihi ya Kiafrika huandikwa tu kwa lugha za Kiafrika"

*- Ngugi wa Thiong'o, Decolonising The Mind (1986)*




Ngugi wa Thiong'o, mwanafasihi na mwandishi wa tamthilia kutoka Kenya ambaye alichunguza athari za ukoloni na dhuluma za viongozi wa baada ya uhuru kupitia kazi zake — zikiwemo ile iliyohusu ufisadi aliyoandika kwenye karatasi ya chooni alipokuwa gerezani kutumikia adhabu ya kuwakasirisha watawala — alifariki dunia Mei 28 katika hospitali ya Buford huko Georgia, marekani akiwa na umri wa miaka 87.

Kifo chake kilitangazwa kupitia taarifa za familia, lakini sababu ya kifo haikuwekwa wazi.

Bwana Ngugi, ambaye alifanyiwa upasuaji wa mishipa mitatu ya moyo mwaka 2019, alikuwa akiishi nje ya Kenya tangu mwanzoni mwa miaka ya 1980.

Mara kwa mara alitajwa kama mmoja wa wagombea wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi, na alichukuliwa kuwa mmoja wa waandishi wa Kiafrika wenye ushawishi mkubwa wa kizazi chake. Alitumia hadithi zake — pamoja na lugha alizozitumia kuziandika — kushughulikia uzito wa historia na mapambano ya kisasa.

Bwana Ngugi alibadili uandishi wake kutoka Kiingereza na kuanza kuandika kwa lugha yake ya asili, Kikuyu, kupitia kitabu chake *"Devil on the Cross"*, kilichochapishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1980 kwa jina *"Caitaani Mutharaba-Ini"*, ambacho kinahusu msichana kijana anayekabiliana na maovu ya kijamii katika Kenya ya kisasa.

Hiki ndicho kitabu kilichoandikwa kwenye karatasi za chooni wakati alipokuwa gerezani.

Kilicosababisha yeye kufungwa gerezani ni ushiriki wake katika kuandika tamthiliya ya *"Ngaahika Ndeeda"* iliyojulikana kwa Kiingereza *"I Will Marry When I Want"* — kazi iliyowakasirisha maafisa wa serikali kwa kuangazia tofauti za kitabaka na ufisadi katika maisha ya baada ya ukoloni.

Serikali ya wakati huo chini ya Rais Daniel Arap Moi ilimkamata Ngugi usiku wa tarehe 30 kuamkia 31 Disemba, 1977 nakuwekwa kizuizini bila ya mashtaka katika gereza la Kamiti lenye ulinzi mkali.

**Kwanini aliamua kuandika kwa lugha ya asili?**

Alisema kuwa uamuzi wake wa kubadili lugha ulikuwa sehemu ya tamko kuhusu nguvu ya watu, kwa kutumia lugha ya kundi kubwa zaidi la kikabila nchini Kenya — Wakikuyu.

**Ngugi ni nani hasa?**

Ngũgĩ wa Thiong'o ni mwandishi, msomi na mwanaharakati mashuhuri kutoka nchini Kenya, anayejulikana sana kwa mchango wake

mkubwa katika fasihi ya Kiafrika, hasa kwa kutumia lugha ya Kikuyu na kupigania matumizi ya lugha za Kiafrika katika uandishi na elimu.

**Maisha ya Awali**
Ngũgĩ alizaliwa mwaka 1938 katika kijiji cha Kamĩrĩĩthũ, karibu na Limuru, Kenya. Jina lake la awali lilikuwa James Ngugi, lakini baadaye alibadili jina lake na kuacha majina ya Kikristo kama ishara ya kujikomboa kiutamaduni na kisiasa.

**Elimu**
Alisoma katika Chuo Kikuu cha Makerere (Uganda), kisha akaendelea katika Chuo Kikuu cha Leeds (Uingereza). Aliporudi Kenya, alifundisha katika vyuo vikuu mbalimbali, ikiwemo Chuo Kikuu cha Nairobi.

**Kazi ya Uandishi**
Baadhi ya kazi zake maarufu ni:
Weep Not, Child ya mwaka 1964 – hii ilikuwa riwaya ya kwanza kuandikwa na Mkenya kwa Kiingereza.

The River Between ya mwaka 1965 – ilihusu migogoro ya kitamaduni na kidini katika jamii ya Wakikuyu.

A Grain of Wheat ya mwaka 1967 – ilihusu uhuru wa Kenya na madhara ya ukoloni.

Petals of Blood ya mwaka 1977 – riwaya kali inayokosoa ubepari na unyonyaji wa wanyonge.

Devil on the Cross" 1980 – aliandika akiwa gerezani; kazi hii iliandikwa kwa Kikuyu (Caitaani Mũtharaba-Inĩ).

**Kifungo na Uhamisho:**
Mwaka 1977, baada ya kushiriki katika uandishi na uzinduzi wa tamthilia ya Kikikuyu iliyoitwa *Ngaahika Ndeenda* (I Will Marry When I Want), serikali ya Kenya ilimkamata na kumweka gerezani kwa zaidi ya mwaka mmoja bila kufunguliwa mashitaka.

Baada ya mateso na vitisho, alikimbilia uhamishoni Marekani, ambako alifundisha katika vyuo mbalimbali, ikiwemo Yale, New York University na baadaye Chuo Kikuu cha California, Irvine.

**Maono na Ujumbe:**
Ngũgĩ ni mfuasi mkubwa wa nadharia ya "uhuru wa kiutamaduni", na anasisitiza kuwa ukombozi wa kweli wa Afrika hautapatikana hadi Waafrika waanze kuthamini na kutumia lugha zao wenyewe katika elimu, fasihi, na mawasiliano ya kila siku.

**Tuzo na Heshima:**
Ngũgĩ ametunukiwa tuzo nyingi za kimataifa na mara kadhaa amekuwa akitajwa kuwa mshindani wa Tuzo ya Nobel ya Fasihi.

Tuzo hizo ni pamoja na
1. UNESCO First Prize (1966) - kwa riwaya yake ya kwanza ‘Weep Not Child’
2. Lotus Prize for Literature (1973)
3. Paul Robenson Award (1992)
4. Pak Kyong-ni Prize (2016) - Tuzo ya fasihi Korea Kusini yenye thamani ya $90,000
5. PEN/Nakobov Award for Achievment in International Literature (1922) - Tuzo ya kifahari kutoka PEN America
6. Premi Internacional Catalunya (2019) - katika kukuza fasihi na haki za binadamu
7. Erich-Maria-Remarque Peace Prize (2019) - kwakupigania haki na amani.
8. Fonlon-Nicols Prize
9. Tähtifantasia Award (2008)
10. Man Booker Internationa Prize (2021)

Pamoja na tuzo hizi baadhi tu, Ngugi alitunukiwa shahada kadhaa za heshima na vyuo mbalimbali huko America na kwingineko. Hii inaonesha jinsi alivyotambulia kimataifa kwa mchango wake mkubwa katika fasihi, lugha, na harakati za kijamii. Kwa kazi zake aliendelea kuwa sauti muhimu ya Afrika katika jukwaa la Kimataifa.

*Imeandaliwa na Amata Ric*

SALUM MAKAMBA

# USHAIRI NI BAHARI SI KIJITO - 01 -

Hivi karibuni palianza kuzunguka mitandaoni picha mjongeo iliyorekodiwa Septemba mwaka 2010 ikimwonesha mwanazuoni na mshairi tajika wa Kenya, Hayati Prof. Ahmed Sheikh Nabhany akizungumza kadha wa kadha kuhusiana na tungo za Kiswahili.
Katika picha mjongeo hiyo, miongoni mwa anayoyazungumza Prof. Nabhany ni sharia za kutunga tungo ambazo anabainisha wazi kuwa ziliibuka baada ya makubaliano ya watu wa Lamu, Pate, Siu na "baadhi" ya watu wa Mombasa.

Kitendo cha neno "baadhi" kutumika ni ishara kuwa kuna watu wengine kutoka Mombasa ambao hawakukubaliana na sharia hizo. Miongoni mwa sharia ambazo Prof. Nabhany anasema watu wa maeneo niliyoyataja hapo juu walikubaliana ni hii isemayo *(nanukuu kama ilivyotokea katika ukurasa wa Ibn Hussein);*

'Shairi ni bahari moja tu: Shairi ni mishororo minne.(4)
Shairi ni liwe na kina na mizani huwa 16/ bi maana kila kipande cha shairi kati ya utao na ukwapi liwe na mizani nane(8). Na shairi ni liwe la lugha ya kiufundi, kimafumbo si lugha nyepesi .

Na shairi zuri ni kati ya ubeti mmoja paka kumi ikizidi kumi na moja, mbili zaidi ya hapo litachosha.. Litakosa wa kulisoma…' Mwisho wa kunukuu.

Baada ya kulisoma andiko hilo la Ibn Hussein ambalo lilitokana na maneno ya Hayati Prof. Nabhany nikaenda katika uwanja wa komenti na kuandika yafuatayo;

"Ukimsikiliza Profesa anasema wazi mwanzo kuwa hayo yalikuwa ni makubaliano yaliyofikiwa na wanazuoni/washairi wa Pwani. Kwa maana hiyo si sheria ya dunia. Kuna watu (nikiwemo mimi) tunaoamini katika ushairi huru. Tunayakubali na kuyatunga mashairi yenye sifa alizozisema Profesa lakini pia na mengine yasiyofuata sifa hizo lakini tunaamini yana uwezo wa kuamsha hisia na kutoa ujumbe ufaao kwa jamii. Kwa mfano, katika Diwani yangu ya Mamangu Nipe Wosia kuna utunzi unaitwa Mamangu Niambie Koma lina mishororo minne, mizani 16 (nane katika ukwapi na nane katika utao) lakini halijatumia lugha ngumu na lina beti 100. Ujumbe lilioubeba una maana kubwa kuliko sheria ambazo zingezuia kuandikwa kwake.

Ninachotaka kusema ni kwamba, washairi wazingatie na kufuata kanuni hizo lakini zisiwabane. Wakiona kuna ujumbe muhimu wa kufikishwa kishairi lakini hauingii katika sheria hizo wasiutie mchagoni. Waandike na kuuleta nasi tutaupokea hivyohivyo. Ushairi ni mpana sana."

Baada ya komenti hiyo wakaibuka watu wa namna mbili. Walioshangaa kwa shairi kuwa lenye beti mia (si utenzi) na waliokuja na hoja kuwa hakuna shairi la namna hiyo na nikaambiwa nauchezea na kuunajisi ushairi.

Binafsi nilitaka nitoe elimu palepale juu ya wapi, kwa nani na nani ambapo nimetoa elimu hiyo na kanuni hizo za kutunga utungo wenye beti zaidi ya kumi na moja na hadi mia na kuuita ushairi na si hivyo tu bali hata tungo zisizo na vina na mizani kisha nikaziita mashairi. Lakini ashakum si matusi, aliyekuwa ananituhumu ameshakaririshwa na hakuwa tayari kujifunza elimu mpya.

Kwa mantiki hiyo nimeamua nitatoa elimu hapa kwa ufupi nikiambatanisha na ushahidi wa wanazuoni juu ya tungo ya beti mia kuwa shairi na tungo zisizofuata vina na mizani nazo kuwa ni mashairi.

Lengo ni kuwaelimisha watu wenye fikra huru watakaokuwa tayari kuelewa lakini pia kuwaondolea shaka wasomaji wa Diwani ya Mamangu Nipe Wosia ili wasije kudhani wanasoma baadhi ya vitu visivyo na hadhi kwa mitazamo ya baadhi ya watu wenye misimamo ya kihafidhina na ufinyu wa fikra kwa kutotaka kujifunza mapya baada ya kukaririshwa katika viambo vyao.

Tukutane toleo lijalo kwa elimu zaidi…

*Kutoka mtandaoni!*

# SAKO KWA BAKO:

## CLEMENTINA 'SE'MBEDULE' – MKULIMA, BANATI ASIYEACHA KITABU

Karibu tena katika safu yetu ya Sako kwa Bako, majuma mawili yaliyopi nilikuwa kirandaranda mitaani katika mkoa wa Iringa ambako ndiko hasa ninapatikana. Katika pitapita zangu hizo nilijikuta katika kitongoji kimoja kinajulikana kama Kinegamgosi jirani kabisa na Ipogolo.

Hapa navutiwa na binti mmoja wa makamo hivi akiwa kwenye shamba la mahindi na kiroba chake ambacho kilijaa mahindi nusu. Kiliconivutia ni kuwa alikuwa kasimama na kitabu mkononi pake akisoma.

"Shikamoo" aliniamkia baada ya kuona nimeruka mtaro na nikimwelekea yeye.

**Marahaba… nimevutiwa na kitabu unachosoma!" nilipomwambia hilo, akakifunga na kunikazia macho. Huyu ni nani?**

Naitwa Clementina Mbedule, naishi hapa Kinegamgosi, nyumba ile paleee! (akanionesha nyumba)

**Nimekuona na kitabu na ndicho kilichonivutia kwako, kitabu gani hicho? Nikamuuliza.**

Akainua mkono wake na kukitazama huku na huku kana kwamba ndiyo mara ya kwanza anakiona.

Hiki ni Uchawi wa Mchungaji Stefano, lakini kidogo tu, kuna kurasa hazipo kabisa.

**Unapenda kusoma vitabu?**

Heeee, wa mimi huyu? Napenda sana sana sana.

**Ilikuwaje ukapenda kusoma vitabu?**

We mi mtoto wa mwalimu mstaafu. Nyumbani kuna vitabu vingi sana. Nilikuwa nasoma kimoja kimoja, yaani vingi. Vya hadithi, vya dini, mashairi na vya kilimo.

**Upo darasa la ngapi?**

Nimemaliza mimi kidato cha nne hapo Tagamenda.

**Ulichukua mchepuo gani?**

Arts. Mi nimesoma arts, na kilichonivutia zaidi ni vitabu. Nyumbani kwetu wote tunesoma Arts na baba ni mwalimu wa Kiswahili. Daima alikuwa anapenda kutusimulia hadithi zilizo kwenye vitabu, nilikuwa napenda sana. Mimi siwezi kukaa mbali na vitabu maana napenda. Hivi hapa mama akinikuta nasoma ugomvi.

**Hapendi?**

Siyo hapendi, ila anataka ufanye kazi kwanza hayo ya kusoma baadae.

**Vitabu vinakusaidia nini?**

Aaa mambo mengi tu najifunza, najifunza tamaduni, kilimo, mapishi yani mengi tu. Unaona hili shamba hapa (ananionesha) hiki kiploti hiki cha kwangu, nimejifunza kwa kusoma kwenye vipeperushi vya mradi wa (akataja huo mradi) walivileta nikaomba na mbegu wakanipa. Nikasoma maelezo yao, namna ya upandaji nikafanya hivyohivyo.

**Hongera sana Clementina… unawaambia nini wengine?**

Mimi nawaambia tu wapende kusoma sana vitabu waburudike na wajifunze. Kwa wanafunzi wa masomo ya arts wasome vitabu ili kujibu maswali vizuri wasitegemee vipamfleti vilivyochambuliwa tayari ni uvivu.

Mazungumzo yangu na binti huyu yalichukua kama dakika kumi na tano hivi. Alikataa kabisa kupiga picha akidai kuwa hajajiandaa na ni mchafu yuko shambani. Sikumlazimisha. Lakini kutokana na mapenzi yake ya vitabu, nimemuahidi kumpelekea vitabu vingine kutoka mradi wa Kitabu Maisha na kumuandikisha kama mwanachama kwenye maktaba ya Mkoa.

Je wewe wapenda kusoma vitabu?

Kitabu ni mkombozi, kamata kitabu, soma, jifunze.

RM

# MSALITI - 04

Na. Richard Mwambe

*Ilipoishia ….*

*"Najua, lakini tutaona jinsi ya ku -deal nao, mipango yetu lazima iende kama tulivyopanga, haiwezi kubadilika!" yule Makamu wa Rais akawaeleza. Baada ya saa moja ya kikao kile kumalizika na mikakati stahiki kupangwa, hatimaye kilifika tamati. Kila mmoja akatakiwa kuondoka na kuendelea na majukumu yake*

*Endelea…*

KAMANDA Amata alivua glavu zake na kuzitundika kwenye henga mahsusi iliyopo hapo jirani kabisa na mlango wa kuingilia Ofisi Ndogo. Nalo koti lake kubwa alilivua na kulitundika papohapo. Akavuta hatua hadi kwenye jokofu na kutoa kibweta kilichojaa vipande vya barafu. Akavitia kwenye bilauri na kisha akatungua chupa ya VAT 69 na kujimiminia. Akainua ile bilauri na kuvuta hatua hadi kwenye kiti kimojawapo ambacho kilikuwa jirani kabisa na dirisha. Akasogeza pazia na kuruhusu macho yake kutalii eneo lote la mbele ya jengo tukufu la Ikulu. Akapiga funda moja na kukunja uso kidogo, kisha akaendelea kutazama yanayoendelea.

Hakukuwa na la zaidi, isipokuwa shughuli za kila siku za wananchi zilikuwa zikiendelea. Na wakati huo Amata alifahamu wazi kuwa mkuu wa nchi yupo ndani ya jengo hilo akiendelea na majukumu yake ya kila siku. Aliitazama saa yake, ilikwishatimu saa tisa alasiri.

Muda wa kuingia mtaani sasa! Akawaza.

Alipomaliza kinywaji chake na kuirudisha ile bilauri mahali pake akalifunga lile pazia na kutoka mule ofisini. Mvua ya rasharasha bado ilikuwa ikiendelea wakati yeye akiingia kwenye gari lake tayari kutoka. Siku hii Jeshi la Wananchi lilikuwa likiiaga miili kumi na nne kati ya kumi na sita ya wapiganaji wa Kitanzania waliokufa huko Beni katika nchi ya Kongo wakiwa katika jukumu la kulinda amani. Pia yeye alikuwa mmoja wa wageni waliokuwa katika uwanja wa Jeshi wa Lugalo jijini Dar Es Salaam. Familia zilipochukua miili yao na kwenda kuendelea na taratibu nyingine, yeye alichukua muda huo kurudi ofisini. Maswali kadhaa alikuwa nayo kichwani lakini hakukuwa na mtu wa kumuuliza wala kumpatia majibu. Akawasha gari na kuliondoa pale maegeshoni. Kwa mwendo wa taratibu akakamata barabara ielekeayo Ocean Road ambayo inapita kando kando mwa ukuta wa Ikulu. Dakika tatu baadaye alikuwa tayari mitaa ya Upanga Sea View.

Haikumchukua muda kuwasili nyumbani kwake Kinondoni mtaa wa Tunisia. Akaegesha gari na kuteremka kuuendea mlango wa mbele wa nyumba ile. Kabla hajaufungua alisimama kwanza na kuutazama kuanzia juu mpaka chini. Alitaka kuhakikisha kama hakukuwa na wageni au la. Palikuwa salama. Akatumbukiza ufunguo na kuufungua ule mlango, kisha akajitoma ndani na kuufunga nyuma yake. Moja kwa moja alifikia jikoni ambako alitafuta chochote cha kula kabla ya kurudi tena sebuleni. Lakini akiwa katika kufanya hayo yote, simu ya sebuleni kwake ikaita kwa fujo. Si mara nyingi simu hii kuita, lakini siku hii hata yeye alijikuta moyo ukimlipuka kwa mwito huo.

Nani huyo anayepiga? Akajiuliza kabla ya kwenda kuichukua. Akaiacha. Lakini baada ya sekunde tano hivi ikaita tena. Akaiendea na kuinyakua kutoka kwenye kile kikalio chake. Akaiweka sikioni. Hakuongea chochote badala yake alikuwa akisikiliza mihemo ya mtu aliyekuwa upande wa pili. Mtu yule alihema kana kwamba anakimbizwa au anauoga wa jambo fulani.

"Na-na-nataka nikupe habari!" yule mtu aliongea huku akiendelea kuhema kwa nguvu.

"Habari gani?" Amata akamwuuliza.

"Ssss-siwezi ku-se-ma kwenye si-simu!" akaongea kwa taabu kidogo. Amata hakuelewa kama mtu huyo alikuwa katika mateso makali au alikuwa katika hali gani.

"Wewe ni nani?" akamuuliza.

# MSALITI - 04

“B-b-b-bbesta Elk..” yule mtu hakumaliza kujitambulisha, ile simu ikakatika.

“Shiiit!” Amata akang’aka. Bahati mbaya sana ile simu aliyotumia haikuwa inahifadhi taarifa za miito iliyoingia wala iliyotoka. Besta anataka kunipa habari! Besta gani na habari gani? Akajiuliza.

Akabaki kaikamata ile simu mkononi kana kwamba kuna nyingine itaingia muda huo. Tayari akili yake ilikuwa ikiruka huku na huko kufikiri juu ya mtu huyo ambaye alijitambulisha kwa jina moja tu ‘Besta’ kabla simu ile haijakatwa. Akaitua na kuirudisha mahala pake. Akaingia maliwato na kuoga vizuri. Ijapokuwa alirudi ili apate muda wa kulala na kupumzika lakini alijikuta tayari akili yake ikitaka kujua kuhusu huyo Besta. Aliamua kutoka. Akavaa tracksuit yake yenye nembo ya Taifa upande wa kulia wa kifua na upande mwingine nembo ya TAKUKURU. Akaiendea pikipiki yake kubwa na kuiwasha. Ni muda mrefu hajatumia chombo hiki. Amata aliiacha nyumba yake na kuondoka. Ilikuwa tayari saa tatu usiku.

❦

Safari yake iliishia Victoria, nyuma ya Hospitali ya International Eyes. Akahesabu geti la kwanza, la pili. Alipofika la tatu akasimama na kuzima ile pikipiki. Akaliendea geti na kugonga. Dakika moja baadaye, mlinzi alifika kuupokea ugeni huo.

“Nimemkuta Mzee Mukhsin?” akauliza mara baada ya kusalimiana naye.

“Ametoka, yupo mkewe” yule mlinzi akajibu.

“Naweza kumwona hata yeye? Mwambie ASP Jaffari kutoka Central ana shida,” Amata akamwambia yule mlinzi ambaye alionekana kubabaika mara tu aliposikia cheo hicho.

“Ka-ka-karibu ndani, pita!” yule mlinzi akashikwa na kigugumizi cha dharula. Amata akaingia hatua moja tu na kusimama wakati yule mlinzi akiielekea nyumba ile. Kweli, dakika kama moja na nusu hivi alitoka mwanamama wa makamo. Amata akamwamkia na kujitambulisha.

“Nina shida na Mzee Mukhsin…” akamwambia yule mama.

“Mzee Mukhsin ametoka, kaniaga anaenda huko Kona Lounge Masaki,” yule mama akamjibu Amata.

“Ok… naomba mpigie mwambie ASP Jaffari wa Central anataka kumuona, ikibidi nikakutane naye hukohuko…” akamwambia yule mwanamama. Hakuwa na maswali mengi, yule mama akaruda ndani na alipotoka, akamwambia “Sawa, amesema anakusubiri!” wakaagana.

Kona Lounge ilimpokea Amata dakika kumi na tatu zilizofuata. Nje ya Lounge hiyo palijaa magari ya kila aina. Ungeyaona tu ungejua eeeeenh hapa ni pa wazito. Aliegesha pikipiki yake na kuingia ndani. Humu Amata hajawahi kuingia pamoja na uzururaji wake wote hapo mjini. Haikumchukua muda kukutana na mwenyeji wake, Mr. Mukhsin. Wakachukuzana pembeni na kuketi.

“Niambie kijana!” Mukhsin akaanzisha mazungumzo. .

*Itaemdelea….*




Kitabu MSALITI kipo madukani, jikamatie nakala yako kwa Tsh 15,000 tu.

Tembelea duka la Kona ya Riwaya Kinondoni au piga

**simu namba 0655428085**
**Whatsapp 0766974865**

Jikamatie nakala yako sasa

# HADITHI: Najutia Kuwa na Wewe—03

**MTUNZI: ASHA SIRAJ**
**Whatsapp 0789044345**



**UTANGULIZI**

**Mapenzi sio kitu cha kuwekea maanani sana kwasababu ipo siku yanaweza kukuletea shida huko mbeleni, kuna baadhi ya changamoto nyingi hutokea. Hivyo ukisema kila jambo uliwekee maanani basi mapenzi yako yatabaki kuwa na majuto siku zote. Kutana na binti SHAZMA aliyepitia mateso mengi kwenye mapenzi yake na kujikuta akijutia kwanini amkabizi moyo wake mwanaume asiye na fadhira**

***lipoishia…***

***Ukweli nilihisi kuzimia kwa maneno ya shangazi, hivi huyo Nishangazi yangu ninayemjua mimi au, kipindi nikiwa mdogo sana kabla ya wazazi wangu hawajafariki alikuwa ananipenda sana nilishangaa sana kumuona hivi sikutegemea kabisa.***

***Endelea...***

SHAZMA hufai kabisa kuletewa vitu vizuri kama hivi, hivi vitu alifaa apewe mwanangu na wala sio wewe mchawi mkubwa wewe.
Mambo ya uchawi tena shangazi nilimuuliza huku nikiwa namuangalia machoni mwake, ndio wewe huna tofauti na mchawi kwanza nahisi wewe ndo mtu uliyemroga binti yangu mpaka kuchukua nafasi ya mwisho darasani.

Shangazi mtu kama hana akili hana tu na wala sio sijui karogwa tokea hapo huyu akili alikuwa hana, hata kabla yangu mimi kuja hapa matokeo yake yalikuwa ya hivi hivi tu siko zote mimi sioni kitu kilichobadilika kwake, japo mmejaribu kumhamisha baadhi ya shule ila hizo ndo akili zake.

Na wala sio kusingiziwa kurogwa hapa. Shangazi alinipiga kibao, chunga mdomo wako we mbuzi unathubutu vipi kumwambia mwanangu hana akili,
Munira aliongea aliyekuwa busy akitazama katuni, mama kila siku nakwambia huyu Shazma aondoke humu ndani ila hutaki kunielewa unaona ni jinsi gani anavyonidhalilisha kwanza sina hata amani akiwemo humu ndani.

Baada ya shangazi kunipiga vibao vya mgongoni niliondoka zangu huku nalia nikielekea chumbani kwangu, nilitamani ningelikuwa walau na picha za wazazi wangu, walau hata niwaone kwa picha.
Ila ndio kama hivyo kila kitu kiliungilia humo ndani hamna hata kitu kilichoweza kupona, nililia sana hadi kupelekea macho yangu kuvimba hata hamu yakufanya kazi sikiwa nayo.
Siku zilizidi kusonga mbele ila mateso ndani ya familia hiyo hayakuweza kupungua, kipindi hicho nilikuwa nau mri wa miaka kumi na tatu naelekea kumi na nne na dada angu Munira alikuwa na miaka kumi na nne.
Siku zilizidi kusonga mbele mpaka pale nilipoweza kuzoea hali hiyo ya maisha yangu, nilikuwa naamka kuswali swala za usiku kwa ajili ya kuwaombea wazazi wangu huku walipo waweze kupumzika kwa amani.

Siku moja yalikuwa majira ya saa saba mchana siku hiyo ilikuwa *weekend* hatukuwa tunaenda shule, hivyo nilienda kutia udhu kwa ajili ya sala ya mchana.
Nilianza kuswali na baada ya kumaliza kuswali nilinyoosha mikono yangu juu nikimuomba Mungu wangu aweze kunisaidia na kunitoa kwenye wakati mgumu ambao naupitia kwa kipindi hicho.
Ila ajabu sauti ya shangazi yangu ilisika kwa nyuma akisema, huyu unayemuomba angekuwa mtu wa kutoa msaada basi angeweza kuwarudisha wazazi wako.
Ingelikuwa vizuri muombe aweze kuwarudisha wazazi wako ili uweze kutupunguzia bajeti maana humu ndani unakula sana mpaka tumeshindwa kukuvumilia, toka uje wewe humu ndani vitu vinawahi kuisha kwa uharaka sana kutokana na ulaji wako mkubwa uliokuwa nao.

Nilishangazwa sana na maneno ya shangazi hata robo ya mchele sikuwa naimaliza iweje mimi ndiye ni-

nayemaliza chakula haraka humu ndani.
Nilishindwa hata kuendelea kuomba nakuamua kumgeukia shangazi yangu. Shangazi ina maana hata wewe humuamini Mungu, bila huyo Mungu basi usingeweza kula shangazi maana yeye ndo mgawa riziki.
Kama mgawa riziki kwanini asiwe anakupa chakula cha kwako pekee ako mpaka usubiri tunachopika sisi, yeye si mgawa riziki si ndio mwambie akupe hata riziki akujengee nyumba yako na uweze kuondoka humu ndani.
Nilijuuliza maswali mengi hata shangazi hamuamini Mungu, nilimtazama sana pasipo kummaliza, hivi huyu ni shetani au jini labda maana hata jini pia hawezi kuongea maneno mazito juu ya Mungu wake.


Ukweli niliondoka sehemu hiyo, hata furaha nilikosa ghafla kwa sababu mimi nilikuwa mtu wa dini sana hata hivyo nilipoona mtu anamzungumza vibaya kuhusu Mungu, nilipenda sana kumuhusia mtu ila nikiona nakusihi sana ukawa mtu ambae hanielewi huwa nakuacha na kuandoka .
Nilifanya hivyo kwa shangazi kwasababu nilihisi kabisa napoteza muda wangu, kwasababu alionekana kuwa mbishi sana kwenye suala la kumuabudu Mungu
Niliendelea na kazi zangu za hapa na pale shangazi alielekea sebuleni alipokuwa amekaa Munira akiangalia tivii, akili za Munira ziliishia kwenye katuni, hata shangazi alisema Munira amerogwa nilimshangaa wakati anajua kabisa akili za binti yake ni katuni.
Sikuwahi kuruhusiwa kuangalia tivii, isipokuwa mume wa shangazi akiwepo ndipo nilipata muda wa kuangalia tivii, alikuwa anafanya kazi serikalini hivyo alikuwa mtu wakuondoka asubuhi kurudi jioni.
Nilipata mda wa kuangalia tivii pindi alipokuwa anarudi kutoka kazini, kwa sababu yeye ndiye mtu aliyekuwa ananinitetea kila wakati, hakupenda kabisa kuona napitia wakati mgumu, hata shangazi yangu alipoweza kunigomba na kunifokea basi yeye aliingilia kati na kuzuia mfarakano huo.

Miezi ilisonga mbele na mtihani wa kumalizia elimu ya msingi uliwadia hivyo nilikuwa mtu wa kuamka usiku nakujisomea maana sikupenda kuona narudia darasa. Baada ya siku kadhaa kupita hatimae siku ya sisi kufanya mtihani iliwadia, tuliriport shule mapema siku hiyo kwa ajili ya maandalizi ya mtihani wa mwisho
Nashukuru Mungu tuliweza kumaliza mtihani wetu vizuri bila vurugu yoyote ile. Baada ya mitihani kuisha tuliruhusiwa kurudi nyumbani huku tukigonjea *graduation* yetu
Baada ya wiki mbili tukiwa nyumbani huku tukisubiri *graduation* yetu hivyo shangazi alikuwa mtu wakunifanyisha kazi, nilitamani bora ningeendelea kuwa shule.
Nilifika mda nikatamani kwenda makaburini kwa wazazi wangu walau niweze kuwaomba wafanye chochote juu yangu mimi, ila sikuwa na nauli ya kutoka hapa hadi Morogoro hivyo iliniradhimu niendelee kuvumilia zile shida ambazo nilikuwa napitia hapo kwa shangazi walau niweze kufikisha malengo yangu
Nilipenda sana kusoma walau huko mbeleni nije kuwa na elimu yangu ili niweze kutoka kwenye maisha ya masimango ya kila siku

Hatimae siku ya *graduation* iliwadia kama unavyojua 'graduu' zilivyo watu wengi walikuja pale japo mimi sikuwa na furaha haswa pale nilipokumbuka miezi mitatu yote nitakuwa pale nyumbani kwa shangazi
Ndipo nilihisi kuchoka nakujiona ni mtu nisiye na bahati kwenye maisha yangu siku hiyo iliweza kupita na *graduation* ilienda vizuri japo hiyo siku mimi sikuwa na amani kabisa
Nilitamani nipate likizo walau ya kuondoka pale miezi miwili mitatu mpaka pale shule zitakazoweza kufunguliwa, na sikuhofia kuhusu swala la mimi kufaulu. Nilikuwa na imani matokea yangu yatatoka vizuri hivyo sikuwaza jambo hilo

Kutokana na mwili mnene niliokuwa nao basi nilioneka mkubwa japo sikuwa mkubwa miaka kumi na nne niliyokuwa nayo  mtu angeniangalia kwa umakini angezania nina miaka kumi na sita hivi

*Itaendelea...*



# Ya Kale Ni Dhahabu– Alibaba na Wezi 40 (19)

Bado kulikuwa na hazina nyingi sana katika pango. Lakini hili halikumfurahisha. Alikuwa mpweke sana. Kwasababu watu wake wote waliuliwa kule kwa Alibaba. Hakuwa na mtu wa kuongea nae – hakuna mtu wa kumuheshimu – wala hakuna mtu wa kumwambia maneno mazuri. Alibaki tu kufikiria kwamba, ni lazima amuue Alibaba!!!!!


Hivyo basi kiongozi wa wezi alikaa pangoni kwa wiki kadhaa akitengeneza mpango mwingine.

"Lazima niwe mwerevu sana," alijisema mwenyewe. "kuna mtu katika ile nyumba ni mwerevu pia. Na ndio maana sasa niko hapa peke yangu. Sasa lazima nifanye urafiki na Alibaba. Kwa njia hiyo nitaweza kuingia ndani ya nyumba ya Alibaba. Nitamuua hali ya kuwa hakutarajia. Huenda nikaamua wakati tunapata chakula cha jioni."

Kiongozi wa wezi akaamua kujifunika uso kiasi ambacho hakuna mtu ndani ya nyumba ya Alibaba angeweza kumtambua. Alivaa ndefu za bandia na akanyoa nywele zake zote na kuwa na kipara.

Kisha, kiongozi wa wezi akaamua kutumia dhahabu zake kununua duka kubwa pale mjini. Akaanza kulijaza duka lake vitambaa mbalimbali vya hariri alivyokuwa amevihifadhi pangoni. Watu wengi sana walikuja dukani kwake na kununua vitambaa vile vizuri. Na muda mfupi tu kiongozi yule wa wezi akawa maarufu sana kama mfanya biashara mkubwa wa kuuza vitambaa vya hariri. Pia alijipatia jina na kujiita: Khoja Hussein.

Alipokuwa akiuza vitambaa kwa wateja wake, alikuwa pia akiwasikiliza



wakizungumzia kuhusu watu tofauti wa pale mjini. Vilevile alifanya urafiki na wafanya biashara wakubwa wa pale mjini. Alitaka kwa hali yoyote ile kufahamu kwa undani kuhusu Alibaba na watu anaoishi nao katika ile nyumba. Siku moja alikwenda kumtembelea mfanya biashara mdogo wa mazulia aitwae Khalid. Duka la Khalid lilikuwa mtaa mmoja na duka lake.

"Habari za asubuhi," Khoja alimsalimia kijana yule. Khalid alikuwa akikunjua zulia refu jekundu akimuonesha mteja wake pale dukani.

"Jina kangu ni Khoja Hussein na ni mgeni hapa mjini. Naona una mazulia mazuri sana!"

"Ahsante," kijana alijibu. "Baba yangu mkubwa Kassim alianzisha biashara hii, lakini alikuja kuuawa katika mazingira ya kutisha sana."

"Heh! Na ilikuwaje ikawa hivyo sasa?" Khoja aliuliza.

"Aliuliwa na wezi msituni!" Khalid alielezea.

Khoja alisogea mbele kidogo na kuonesha mshangao usoni.

"Kifo cha kutisha!" alisema. "umesema alikuwa ni baba yako mkubwa – ina maana ni kaka wa baba yako?"

"ndio," Khalid alijibu.

"Na je baba yako yuko hai leo?" Khoja aliuliza.

"Oh , ndio," Khalid alijibu. "Ninaishi naye sasa pamoja na mama yangu na mama yangu mkubwa ambaye ni mke wa marehemu baba yangu mkubwa."

"Na baba yako anaitwa nani?" Khoja Hussein aliuliza.

"Jina lake ni Alibaba!" Khalid alijibu.

Siku inayofuata, Khoja Hussein alirudi pale dukani kwa Khalid.

"Nilifurahia mazungumzo yetu jana," alimwambia muuza mazulia. "nafikiri tunaweza tukawa marafiki wazuri sana. Unaweza ukaja kwangu kupata chakula cha jioni leo."

Hivyo wawili hao walipata chakula cha jioni pamoja na baada ya hapo wakawa ni wenye kuonana kila siku. Wakati mwingine Khalid alikwenda kwenye duka la Khoja Hussein na wakati mwingine Khoja Hussein alikwenda kwenye duka la Khalid na kuzungumzia mambo mbalimbali yahusuyo vitambaa vya hariri na mazulia na kuhusu wateja wao.

*Itaendelea...*



# TAMASHA LA TANZANIA FASIHI FUND 'TAFF' MSIMU WA TATU LAFANA

## 'Rudisha Kitabu Nyumbani…'



**Na Mwandishi wetu**

TAFF ni taasisi inayoiweka fasihi ya Kiswahili katika mwonekano wa pekee Tanzania na Afrika Mashariki.

Msimu wa tatu wa tamasha la TAFF umetamatika pale Kijiji cha Makumbusho ya Taifa, Kijitonyama tarehe 29 ya Mwezi Mei. Ulikuwa msimu wa tatu baada ya ule wa kwanza kule Kisarawe uliobeba kauli mbiu 'Kusoma Siachi Ng'o!' na ule wa pili uliobeba kauli mbiu 'Kitabu Kila Mahali' na huu sasa ulibeba kauli mbiu matata kabisa yenye ujumbe mzito kwa jamii 'Rudisha Kitabu Nyumbani'.

Katika tamasha hili lililokusanya watu takribani 300 wakiwemo wanafunzi wa shule ya Msingi katika viwanja hivyo liling'oa nanga siku ya tarehe 28 Mei kwa burudani moto moto na salamu mbalimbali kutoka kwa wageni maalum walioalikwa. Pamoja na zilizosheheni vitabu vya kila aina; vya watoto, vya historia na siasa, riwaya na maarifa. Waandishi na wawakilishi wao walipata nafasi ya kuzungumza machache mbele ya Mgeni rasmi na wengine wote.

Siku ya pili ilikuwa ni warsha na mafunzo, kubadilishana mawazo na kuona jinsi gani fasihi itapelekwa mbele zaidi na kuipa thamani kwa waandishi, wasomaji na jamii nzima. Ulikuwa ni wakati mzuri wa kutazama mustakabali wa fasihi na mwanafasihi. Washiriki pia walipata nafasi ya kutembelea kijiji hicho cha makumbusho na kujifunza tamaduni na historia ya Mtanzania. Aidha walijionea nyumba na vitu mbalimbali vya asili ya Mtanzania na mwisho walipata burudani nzito ya ngoma za asili na michezo ya sarakasi kutoka kikundi cha Makumbusho.

"Naweza sema kuwa kupitia tamasha hili nimejifunza kitu kikubwa sana, na ningeomba wakati mwingine tamasha hili lije na kwetu Zanzibar," alisema mmoja wa washiriki yote washindi wa hadithi fupi waliopata nafasi 11 za juu katika shindano lililoandaliwa na taasisi hiyo walikuwapo. Kilichofurahisha zaidi ni kwamba hadithi zote hizo zilichapwa, na vitabu vilikuwapo.

"Katika awamu hii ya tatu tumeendesha mashindano ya uandishi kulenga suala la Bima" alisema Mkurugenzi wa taasisi hiyo Bwana Hussein Wamaywa katika salamu zake za ufunguzi. Pia aliwashukuru TIRA kwa kuchapa vitabu hivyo na alitoa wito kuwa vifikishwe katika maktaba mbalimbali.

Fauka na hayo, katika tamasha hili pia walikumbukwa baadhi ya nguli wa fasihi ya Kiswahili wa Tanzania waliotangulia mbele ya haki; Martha Mvungi, Ben Mtobwa, Ndyanao Baslisidya na mshairi Amir Sudi Andanenga 'Sauti ya Kiza'. Maneno mazito na mazuri yalitolewa juu ya nguli hawa. Kumbukumbu hii nzito ilirudisha huzuni kwa washiriki lakini iliacha fundisho kubwa. TAFF waliigusa upya mioyo ya washiriki.

Washiriki wote walipata nafasi ya ziara ya kifasihi, kutembelea meza moja baada ya nyingine kutoka Zanzibar.

Katika kuhitimisha tamasha hilo, TAFF walitoa tuzo za heshima kwa Hayati Ben Mtobwa, Martha Mvungi, Ndyanao Balisidya na Amir Sudi Andanenga kwamba pamoja na kuwa wametangulia mbele ya haki lakini mchango wao katika fasihi ni mkubwa na athari yake bado ipo hata sasa. Pia tuzo nyingine za heshima zilitolewa kwa watu ambao bado wapo hai, na kwa namna moja au nyingine wanapambana kuipeleka mbele fasihi. Nao walikuwa Omar Baajun, Abdulatif Abdallah, Buinda Mjungu (Msomaji) na Richard Mwambe—Mkurugenzi wa Ngurumo ya Mwandishi.

Kisha wale wote washindi 11 wa hadithi fupi walipatiwa vyeti vya ushindi. Nao walikuwa (kwa majina yao) ni Beda Msimbe, Laurent Fungavyema, Gwamaka Mwamasage, Esuvati Daniel, Lilian Mwita, Walter Yobo, Fatma Suleiman, Odwa Omondi (Kenya), Edwin Omundo, Maimuna Hashimu na Joyce Makajonga.

Ngurumo ya Mwandishi inatoa pongezi za dhati kwa TAFF na inatoa wito kwa vyama vingine kuandaa matukio kama haya ili kuipeleka mbele fasihi ya Kiswahili.

# HISTORIA YA VITABU ULIMWENGUNI—03

**Tunaendelea na andiko letu juu ya Historia ya Vitabu Ulimwenguni. Na katika toleo hili la 43 tunakifikia Kitabu cha Watibeti 'The Tibetan Book'. Haya na tuendelee…**

**The Tibetan Book**

Mara nyingi huwa inahusishwa na vitabu viwili tofauti ambavyo vina athari kubwa katika falsafa ya Kibuddha, hasa ya Tibet, na vimevutia watu wengi duniani kwa sababu ya mafundisho yake juu ya maisha, kifo, na hali ya uhai wa baada ya kifo.

Kuna vitabu viwili maarufu vinavyohusishwa na jina hili:

Hakika! "**The Tibetan Book**" mara nyingi huwa inahusishwa na vitabu viwili tofauti ambavyo vina athari kubwa katika falsafa ya Kibuddha, hasa ya Tibet, na vimevutia watu wengi duniani kwa sababu ya mafundisho yake juu ya maisha, kifo, na hali ya uhai wa baada ya kifo.

Kuna vitabu viwili maarufu vinavyohusishwa na jina hili:

## 1. Kitabu cha Wafu cha Kitibeti 'The Tibetan Book of the Dead (Bardo Thödol)

**Maana:** *"Kitabu cha Wafu cha Kitibet"*
**Lugha ya asili:** Kitiibeti, kilitafsiriwa kwa Kiingereza na Walter Evans-Wentz mwaka 1927.
**Maudhui:**

- Ni mwongozo wa kiroho unaosomewa kwa mtu anayekaribia kufa au aliyekufa.
- Kinaeleza mchakato wa roho kupitia "Bardo" – hali ya kati kati ya kifo na kuzaliwa upya.
- Kinaeleza maono ya miungu ya huruma na ya hasira, ambayo yanatokea kwa roho, na namna ya kutambua hali hizo kama sehemu ya akili yako mwenyewe ili upate ukombozi (enlightenment).
- Lengo lake kuu ni kusaidia roho kupata *moksha* (ukombozi wa kiroho) na kuepuka kuzaliwa tena katika hali duni.

**Mambo muhimu yanayofundishwa:**

- Kutokuwa na hofu wakati wa kifo
- Umuhimu wa kuelewa hali ya akili
- Ukombozi upo ndani ya kutambua ukweli halisi wakati wa hali ya mpito

## 2. The Tibetan Book of Living and Dying

**Mwandishi:** *Sogyal Rinpoche* (1992)
**Maudhui:**

- Ni tafsiri ya kisasa ya mafundisho ya "The Tibetan Book of the Dead", lakini inaongezwa na masimulizi ya kisasa, tiba, na falsafa ya maisha.
- Inazungumzia maisha kwa upana, jinsi ya kuishi kwa hekima, na kujiandaa kwa amani kuelekea kifo.
- Inasisitiza mazoezi ya kutafakari, huruma, na uhusiano wa karibu kati ya maisha na kifo.

## Kwa Nini Kitabu Hiki Ni Muhimu?

- Kinatoa mtazamo tofauti wa kifo – si mwisho, bali ni mchakato wa mabadiliko.
- Kinaweza kusaidia watu wanaohitaji faraja, kuelewa huzuni au majonzi, au wanaotafuta maana ya maisha.
- Kinaweza kuwa chanzo kizuri cha msukumo wa kiroho kwa waandishi, wanamafalsafa, na wale wanaochunguza maisha ya ndani (*inner life*).

**Ikiwa wewe ni mwandishi wa hadithi za falsafa au maisha ya kiroho**, unaweza kutumia falsafa za Bardo na mabadiliko ya roho kama alama (metaphor) ya safari ya mhusika wako – kutoka kwenye giza la kutojua kuelekea kwenye nuru ya kujitambua.

*Katika toleo lijalo tutaangazia kitabu kingine...*

# KITABU NILICHOSOMA

## SHOW YOUR WORK (marudio)

**Jina la kitabu-** Show your work
**Mwandishi-** Austin Kleon
**Msomaji–** Vrom
**Mkoa-** Dar

Mm nimejifunza kwanza ili watu wengine wakuone au wajue unachofanya sio lazima upate *audience* ya watu wakubwa wakusikilize ila ni kujaribu kujitangaza katika hz social media zetu kwa kuzingatia maudhui ya yale unayotaka watu wapokee na kujifunza zaidi kutoka Kwako.

Nimejifunza kuwa huhitaji mtu aku*push* ili uweze kufanya jambo, kinachohitajika ni kusimama, kuamua na kutenda bila kuogopa.

Jambo jingine ni kutokuruhusu roho ya uoga au kukata tamaa, ktk kila jambo lazima tuzingatie wapi tunataka kufika.

Nimejifunza pia katika kila kazi ambayo mtu anafanya lazima apate mirejesho mibaya na mizuri kwa hiyo tusiogope na tusichukulie *personal* maana kila mtu ana upeo tofauti na kuendelea na zile *comment* ambazo zinajenga kusonga mbele.


Nimejifunza kufanya kitu ambacho mimi ninakipenda ambacho nitafanya kwa nguvu zote bila ya kukata tamaa.

Nimejifunza kwamba kujua kitu hakumaanishi ndyo mwisho wa kujifunza. Kila siku tunatakiwa kujifunza vitu mbalimbali vipya ili kuboresha kile ambacho unacho au unakifanya.

Hili ni kubwa kuliko, nimejifunza ku*share* kile kitu ambacho nafanya ili watu wajifunze kutoka kwangu ambavyo itazidi kuonesha uwezo wa kile ninachofanya. Ndyo maana tunaona watu wenye kutoa sana kwa watu huwa wanakua kifikra, wanabarikiwa na kuzalisha zaidi kwasababu wameamua ku*share* na watu wengine.

Nimejifunza pia *work life balance*. Mwandishi anatusisitizia kuwa tuwe na muda wa kufanya kazi na muda wa kufanya mambo mengine kwa ajili ya ustawi wetu wa afya ya akili.

Kwa mfano kama unafanya biashara *then* uwe na muda wa ikizo iwe walau miezi 3 au sita au hata mwaka huku biashara ikiendelea bila kuathirika. Tunaita *having business continuity*. Wateja hawatateseka kupata huduma au bidhaaa.




**Je; wewe ni mmoja wa wanaopenda kusoma vitabu aina mbalimbali? Na hujui wapi au vipi utapata vitabu hivyo?**

**Anna Mbise Mobile Library ndiyo jibu lako. Jiunge sasa na mamia ya wasoma vitabu kwenye Anna Mbise Mobile Library.**

**Ukitaka kuwa mwanachama wa maktaba hii, tuma ujumbe "NIAZIME KITABU" kwenye Facebook Messenger.**

**Au piga simu namba: +255766069962**

Read & Write
With
Anna Mbise













Picha za matukio mbalimbali ya Tamasha la Fasihi lililoandaliwa na Tanzania Fasihi Fund lililofanyia tarehe 28 na 29 ya mwezi Mei katika viwanja vya Kijiji cha makumbusho ya Taifa Kijitonyama, jijini Dar es salaam

**TANGAZA na NGURUMO YA MWANDISHI kwa bei nafuu na ya kirafiki.**
**Matangazo madogo ni Tsh 5000@ na Tangazo la kurasa nzima ni Tsh 10000@.**
**Wasiliana nasi kwa simu *(call & Whatsapp)* 0766974865 na Email: jamvilasimulizi@gmail.com**

## BURIANI WETU NGUGI

Mengi umeyapitia, dunia ni yetu njia
Mengi metuandikia, mafunzo kutupatia
Nchi ukaikimbia, mateso lipozidia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Kikuyu wakulilia, Afrika tweka tanzia
Kalamu loandikia, ukiwa meiachia
Nasi tuloshabikia, twabaki kuangalia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Fasihi lipigania, gerezani kaingia
tamaa hukukatia, chooni kaandikia
Andiko katupatia, maonyo kutuachia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Vitabu lotwandikia, morali metupatia
Mitihani twajibia, vipaji kuchipukia
Hazina umetwachia, Afrika nayo dunia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Tuzo walikutuzia, heshima kukupatia
Afrika yakulilia, mwalimu na mzazi pia
Hili ulotuachia, hakika tapigania
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Twabeba wako wosia, mkoloni mbali tupia
Lugha zetu kukazia, vitabu kuandikia
Shuleni kufundishia, nyumbani kuzitumia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

Tunatangaza tanzia, sikia yote dunia
Mwamba ametangulia, kwa Mola wa Jalia
Sisi twomboleza pia, mahoka wetu sikia
Buriani wetu Ngugi, peponi tutaonana.

***Limetungwa na***
***Amata ga imba***

## NIMUOE AMA NIMWACHE?

Nini niseme usikie?
Kilio gani wataka nilie?
Najua kuwa ni bintie
Nimuoe ama nimwache?

Kwanza hajui jiko
Wala kukalanga diko
Kutwa kucha ni mitoko
Nimuoe ama nimwache?

Kwa sura kasurika
Kwa umbo kaumbika
Tabiaye nataabika
Nimuoe ama nnimwache?

Hajui kutulivika
Ampendaye kumshika
Kitandani patashika
Nimuoe ama nimwache?

Ndoa ajitahidi ishi
Harusi hajui ishi
Hataki pokea michi
Nimuoe ama nimwacha?

Mtaani wanasema
Kaonjwa na kila mwema
Ndani mkaidi nje mama huruma
Nimuoe ama nimwache?

Kama humjui hutomjua
Jukwaale alijua
Shere atakuzuzua
Nimuoe ama nimwache?

Nimuoe ama nimwache, ndilo nalokuuliza
Kwani haya ni machache, juu yake kukujuza
Ndani atemapo cheche, mimi huyo hutereza
Nimuoe ama nimwache?


***Bakari Jamari***
***Mdau wa Ngurumo,***
***Mang'ula.***

**Unaweza kuchangia chochote ili kuwezesha jarida hili kuwa bora na kuwafikia wengi zaidi. Kama upo tayari, changia kiasi chochote kupitia MPESA LIPA NAMBA 5559006 JAMVI LA SIMULIZI. Na Mungu atakujazi.**













Jenga tabia ya kusoma vitabu kila upatapo muda. Vitabu vyetu vinapatikana

Duka la Kona ya Riwaya Kinondoni - Simu namba 0655428085
Posta Mpya Dar es salaam karibu kabisa na mzunguko wa Sanamu ya Askari kwa Joji - Simu 0713454152
Morogoro Morena hotel, Stendi ya Dalala Smaki Samaki na Bima kwa Markus Mpangala - Simu 0719226293
Au wasiliana nasi Jamvi la Simulizi kwa Whatsapp Namba 0766974865

**Hiki ni kitabu kilichoandikwa miaka mingi sana nyuma. Kiliandikwa ili kiweze kusomwa na watu mbalimbali na kuwekwa kwenye maktaba za vijijini. Tunakitoa kutoka kwenye maktaba yetu ili kukupa uhondo, Ngurumo ya Mwandishi ni kisima cha fasihi chenye hazina iliyotukuka.**

## TAMAA YA UTAJIRI WA HARAKA HARAKA—9

### SURA YA 3
### Kisomo na maendeleo kijijini

Hawakuwa na shida ya kuuza mazao yao kwa sababu palikuwa na chama chao cha ushirika ambacho kilinunua mazo ya shamba la kijiji na hatimaye kuuza kwa vyama vingine vikubwa vya ushirika au shirika la usagishaji kwa niaba ya kijiji. Kadhalika Mpepo na wanakijiji wengine waliuza mazao yao kutoka mashamba yao madogo kwenye chama chao cha ushirika - hakukuwa na shida yoyote.

Kwa vile Mpepo alikwishakuwa na shughuli nyingi ilimbidi kugawa muda wake ili asije akachanganyikiwa na kushindwa kutimiza majukumu aliyopewa na kuyakubali yeye mwenyewe. Muda wa shughuli za kilimo aliugawa mara mbili: kilimo katika shamba lake na shamba la kijiji ambalo lilikuwa na ratiba yake kamili. Pia alitenga muda wa kuhudhuria kwenye kisomo. Kisomo chake cha zamani kilikuwa kidogo na kilianza kutoweka hivyo aliamua kujiunga na madarasa ya juu ya kisomo cha kujiendeleza. Pia alishiriki katika kazi za uongozi kuhudhuria vikao na kuongoza mikutano kwa mujibu wa nyadhifa alizopewa.

Pamoja na majukumu hayo aliweza pia kubakiwa na muda wa burudani, kama vile kuangalia michezo, vikiwemo vikundi vya utamaduni kijijini, kusikiliza redio na kadhalika.

Kutokana na shughuli nyingi ambazo baadhi yake zilihitaji kisomo , Mpepo haraka alijiunga na kisomo cha kujiendeleza. Somo alilolipenda zaidi lilikuwa ni Siasa. Alijifunza mambo mengi na maana ya misemo ya kisiasa - wakoloni, itikadi, mabepari, mabeberu, wazandiki, ufisadi, katiba ya chama. Vilevile alijifunza habari za vikao mbalimbali kuanzia shina hadi ngazi ya taifa, katiba ya serikali na vyombo vyake, bunge na mambo mengine mengi.

Pamoja na kujifunza siasa alipata pia mwanga wa Jiografia. Alijua wakoloni walitoka nchi gani na nchi hiyo iko wapi. Katika somo la uchumi alijifunza ni vitu gani hasa mkoloni aliwadhukumu Watanzania hata kuzaliwa kwa neno "Unyonyaji" kwa wakati ule. Hiztoria pia, ilijipenyeza hapa na pale.

Kadiri alivyo alivyoendelea, Mpepo alipatwa na shauku ya kujifunza mambo mbalimbali kwa kutumia maktaba, redio na vikundi mbalimbali vya majadiliano. Katika maktaba hakuweza kupata vitabu vya burudani kama vile hadithi za sungura, hadithi za kienyeji bali vitabu vyenye mada zenye mwelekeo wa masomo maalumu. Wakati mmoja, baada ya kushindwa kujizuia alijisemea mwenyewe: "Kwakweli kuna haja ya vitabu vya burudani kama vile vichekesho, hadithi za wahenga na vituko mbalimbali. Haifai kusoma vitabu vya maarifa tu; tunahitaji kucheka pia baada ya kazi ngumu."

waliomsikia akitoa maneno hayo walimcheka na kudhanisa sasa Mpemo isomo kimeanza kumpeperusha.

Alihudhuria mikutano kadhaa, hasa ile ya shule. Katika vikao vya shule shughuli kubwa ilikuwa kuinua maendeleo ya shule; kuimarisha nidhamu kwa wanafunzi, waalimu na wazazi. Wengi wa wahusika - yaani wanafunzi, wazazi na waalimu waliwahi kuadhibiwa kwa kukiuka majukumu. Mpepo anakumbuka mkasa mmoja uliotokea baada ya kubainika kwa mwalimu mkuu, Mzee panya na Mwenyekiti wao Mama Koroboi.

"Nakumbuka tukio moja baya tulilolishughulikia, nalo ni wakati ambapo mwalimu mkuu alitumia ovyo fedha za shule. Tulianza kumuuliza kwa uungwana baada ya kupata tetesi kutoka kwa wazazi. Tulitaka tupewe jibu la kutosha na kutuondoa shaka kutoka kwake.

***Itaendelea toleo lijalo….***



# ELIMU JAMII

## SAFARI YA MALEZI

**Na Kelvin Kyara**

### 1.1 TONE LA LEO, UA LA KESHO

Malezi ni nguzo ya Maisha, ni kama tone la maji lililopo katika mti mchanga, likiupa nguvu na kuukuza mti huo mchanga ili baadae uje utoe maua mazuri. Hii inamaanisha nini? Tunapotoa malezi bora sasa, tunajihakikishia kesho tutakuwa na kizazi kinachoongozwa na maadili mema, upendo, na bidii. Lakini ikiwa tutayaacha malezi haya kwa udhaifu, tunahatarisha maadili kwa kizazi cha kesho.

Umuhimu wa malezi bora hautakiwi kupuuzwa, mtoto aliyepewa malezi mazuri hujifunza sio somo la kitabu tu, bali somo la maisha. Hujifunza kuwaheshimu watu, kuwa na maadili, kujitambua na kuweza kuchukua maamuzi mazuri katika maisha yake. Lakini kutokujali malezi hali hii huleta madhara makubwa, kwani mtoto anaweza kupotea njia, kuwa na tabia mbaya, na hata kuingia kwenye matatizo kama utoro, uhalifu, uraibu wa dawa za kulevya nk. Katika jamii yetu ya Tanzania tunawaona watoto wengi wakiishi mitaani na kuitwa 'watoto wa mitaani'.

Malezi ya sasa yana changamoto kubwa sana ambayo tusipoizuia sasa italeta madhara makubwa hapo mbeleni, japokuwa hata sasa haya madhara yameshaanza kuonekana, na ndiyo maana tunasikia sana huu msemo, "*Watoto wa 2000*" hii inamaanisha kuwa kizazi hiki kimekuwa na usumbufu, kutokuelewana, na mambo kedekede yasiyokuwa na maadili. Tujiulize swali, je tunatoa malezi bora kwa watoto wetu au tunafuga? Kwa nini nimeuliza *tunafuga?* Ni kwa sababu katika maisha ya sasa wazazi wengi wamekuwa wakiwapatia watoto wao malazi, yaani chakula na mahitaji mengine, lakini mzazi hana muda na mtoto wake. Mzazi anatoka saa 11 asubuhi mtoto hajaamka, anarudi saa 4 usiku mtoto ameshalala. Je tunategemea hapa mtoto anapataje malezi ya wazazi wake?

> ...je; tunatoa malezi bora kwa watoto wetu au tunafuga?

Hii haina tofauti na kufuga ng'ombe, unawapatia chakula tu. Je, ni lini tutayajibu maswali yanayowasumbua watoto wetu, ? Je, ni lini tutafahamu kwamba dada au kaka wa kazi tuliye mwajiri awatunze watoto wetu anawalea vizuri bila ya kuwanyanyasa au kuwafundisha mambo mabaya?

Hili halitawezekana kama hatutatoa muda wetu kama wazazi katika malezi. Tutenge muda wa kuwasikiliza Watoto wetu, kuwachunguza mambo wanayoyafanya nk.

Kila jitihada tunazozifanya sasa, zinaweza kuleta matokeo makubwa mbeleni. Tukumbuke malezi sio jukumu la mzazi pekee, bali jamii nzima inapaswa kuwa sehemu ya safari hii; waalimu, ndugu, marafiki. Malezi ya sasa tumeyaacha katika utandawazi, watoto wanakesha kwenye luninga na simu janja, wanapata maudhui mabovu, kesho na keshokutwa wanaanza kuyafanya hayo waliyojifunza sasa, tunabaki tukilaumu kwamba kizazi cha sasa hakina maadili, lakini tunajisahau kuwa ni sisi wenyewe tumekiharibu.

Pia kuna changamoto hii ya malezi ya mzazi mmoja, ambayo pia imeleta athari kubwa sana kwa ukuaji wa mtoto, kwani mtoto anataka kujifunza na kulelewa na wazazi wote wawili, hivyo katika jamii ya sasa maadili yamekuwa ni changamoto kubwa na kilichosababisha ni malezi mabovu tunayoyotoa kwa kizazi hiki cha sasa.

Nipende kusema malezi bora yanahitaji uvumilivu, na matokeo hayaji kwa haraka. Tukumbuke, hakuna maua yanaochanua bila maji ya kutosha, na hakuna jamii inayoweza ikastawi bila malezi bora ya watoto. Hivyo tunapaswa tufahamu nafasi ya wazazi na walezi katika malezi. Tujue aina ya malezi ya kuepuka, nafasi ya dini katika malezi, nidhamu katika malezi (aina bora za adhabu kwa mtoto), marafiki wa mtoto, malezi katika kukuza ubunifu wa mtoto, madhara ya pombe (ulevi wa mzazi/wazazi) katika malezi na mambo ya kuzingatia katika malezi. Ili tujenge jamii nzuri ya kesho yenye maadili.

*Anasimulia Amata Ric…*

"Kilichonishtua ni ile sauti nyororo ya MC machachari, Eva Mrema ambaye wengi humwita 'Malkia wa Tabasamu' au 'Kungwi' akiwa kando tu ya jukwaa kuu lililobeba wageni mashuhuri kutoka taasisi kubwa kubwa hapa Tanzania. Nilitega vyema masikio yangu kusikiliza ni nini chafanya hata jina langu liungurume kwenye spika kubwa zilizozunguka uwanja ule?

Tanzania Fasihi Fund, katika tamasha lake la fasihi msimu wa tatu uliwatambua na kuwapa heshima watu kadhaa wenye mchango katika fasihi ya Kiswahili. Na Amata Ric Richard Mwambe, nikatajwa. Basi, nilipokea tuzo ya heshima (Ngao maalumu) inayotambulika kama **'Tuzo ya Heshima ya Fasihi ya Kiswahili'** ikiambatana na ujumbe huu…

'Tuzo ya Heshima ya Fasihi ya Kiswahili Imetolewa kwa Richard Mwambe - 'Amata Ric'. Kwa mapenzi, moyo wako wa kujitolea, na mapambano yako ya kuitukuza fasihi ya Kiswahili'.

Lakini pamoja na ngao hii, kilitolewa pia Cheti cha Heshima. Cheti hiki kiliueleza ujumbe ule uliopo kwenye ngao kwa mapana na marefu, ambao ulinitoa machozi. Ulisema hivi…

Cheti Cha Heshima
Kimethibitishwa kwa
Richard Mwambe 'Amata Ric'
Anatunukiwa
**TUZO YA HESHIMA YA FASIHI YA KISWAHILI 2025**

Kwa kutambua na kuthamini mchango wake mkubwa katika kuikuza, kuieneza na kuendeleza Fasihi ya Kiswahili kupitia maandiko yake bunifu ya simulizi, uandishi wa riwaya za kijasusi zenye mvuto wa kipekee kama Tufaa Jekundu, Cronoc 7, Mpatanishi, Harufu ya Kifo, Opereshenі Kashmir na Msaliti.

Kupitia ubunifu wa majukwaa ya Jamvi la Simulizi, Kitabu Maisha na Ngurumo ya Mwandishi, Richard Mwambe ameweza kufungua milango kwa waandishi chipukizi na kuifanya fasihi ya Kiswahili isikike, isomwe na kuheshimiwa ndani na nje ya Tanzania.

Mfuko wa Fasihi Tanzania unatoa Tuzo ya Heshima ya Fasihi ya Kiswahili kama ishara ya kuthamini juhudi hizi ambazo zimeleta mapinduzi chanya katika mazingira ya kifasihi na kukuza upendo kwa lugha ya Kiswahili.'

Ilikuwa ni kitu ambacho sikutarajia, nilipigwa bumbuwazi. Heshima kubwa inayotolewa kwa mtu mdogo. Hapa nilijifunza kitu kikubwa sana kuwa, katika maisha, kila kitu unachokifanya kwa ajili ya jamii, unachokiona wewe kuwa ni kidogo, basi lipo kundi la watu upande wa pili linaloona ukubwa wake.

Haraka sana, mawazo yangu na hisia zangu zilimkubuka Hayati Rey Stanley ambaye mchango wake mkubwa sana uliweza kufanya haya yaonekane. Ningetamani yeye apokee lakini hakuwapo. Apumzike kwa amani.

Ninawashukuru sana TAFF kwa heshima hii, wamenipa heshima mbele ya wapenda fasihi. Tuzo hii inakuwa chachu ya kuendelea na mapambano katika kuipeleka mbele fasihi ya Kiswahili.

Nimepokea salamu nyingi za pongezi, na kati yazo, asilimia mia moja zimesema 'hakika unastahili' asanteni nyote. Bila ninyi mimi si lolote katika fasihi."

*Richard Mwambe*






# HAPPY NEW YEAR '06'—Twahir Yusuph

*Ilipoishia…*

*Mara punde taa zikawaka, zilimshtua na kumfanya atoe sauti ya hofu. Ila muda huohuo alipigwa na butwaa, mbele ya mboni zake walisimama watu wengi aliowashangaa, kila mmoja alishikilia maputo, na ndiyo yaliyokuwa yakipasuliwa na kutoa sauti hizo.*

---

*Endelea…*

Alijifunika uso wake kwa mshangao, zilikuwa familia mbili anazozijua; baba, mama yake, pamoja na wazazi wa Labi Kimati wakiwa na watoto wao wengine. Akiwa kwenye mshangao asiouamini, muda huohuo alihisi kuguswa bega. Vivi aliitoa mikono yake usoni na kugeuka, hichi ndicho kilichozidi kuzibonda hisia zake kwa vikofi vingi vya kimahaba. Alikuwa Labi Kimati aliye na pete viganjani.

"Naomba kuishi kwenye nyumba ya mapenzi yetu milele, mimi tu mmoja, na wewe tu mwenyewe Vivi. Je? Utaolewa na mimi?" ni maneno yaliyosikika vyema kwenye masikio ya Vivi aliyebaki bado haamini kwa yanayomtokea. Machozi yakaanza kumtiririka. Alikuwa akilia kwa furaha Vivi. Akamshika mabega akimnyanyua Labi wake aliyepiga goti, kisha akamkumbatia.

"Nakupenda Labi, nitakupenda milele na zaidi mpenzi wangu." aliongea akilia, huku machozi yake yakiidondokea suti ya mwanaume huyo anayemtakia. Ni Labi wake. Makofi mengi yakapigwa ndani ya sebule la jumba hilo la kifahari. Labi alimshangaza mpenziwe Vivi kwa tukio hilo lililomsisimua pia. Tukio lililoshuhudiwa na wazazi wa pande zote mbili. Lilivutia mno. Labi na Vivi walikuwa wapenzi wa muda mrefu, leo walichumbiana, ikiwa ni moja ya njia ya kwenda kulikatia leseni penzi lao, ili Mungu aliyewaumba awape baraka zake kihalali. Pete ilivishwa kwenye kidole cha Vivi, wazazi wa pande zote mbili wakalibariki tukio hilo, lililoandaliwa kwa kila mtu kujua, kasoro Vivi tu pekee. Alianza Mzee Sesewa Kimati kuzungumza na hadhara mbele ya familia hizo mbili zilizokutana, akafuata Aloyce Cosmas ambaye ni baba mzazi wa Vivi, akina mama nao hawakuwa nyuma, walitoa baraka zao kwa watoto wao hao wanaoikaribia hatua kubwa ya mahusiano yao.

**SURA YA 6**

Wapendanao wakapewa jukwaa waseme chochote, Vivi hakuweza, hisia za furaha bado zilimsisimua binti huyo, machozi yakaendelea kumtiririka, bado alikuwa pembezoni mwa Labi wake, alilia juu ya bega la mpenziwe huyo. Labi hakuwa mvivu kwenye suala linalomuhusu Vivi, alimkumnyata ayuni wake huyo kifuani mwake kwa kum'bembeleza. Kisha akaichukua nafasi hiyo na kuanza kuzungumza yeye.

"Ahsante Mungu, ahsante mno wazazi wetu, shukrani kwa familia zetu zote mbili kwa kukusanyika pahala hapa kwa ajili yetu sisi tu wawili. Huu ni upendo." aliweka tuo. "Nipende kumshukuru pia Vivi, sio kila mtu huwa anapewa nafasi kubwa kama hii kwenye moyo wa mwanamke. Nataka nimwambie kitu, nje ya kumpenda kwangu, mi ni shabiki wa anavyoheshimu hisia zangu, nafurahia sana." alitupa maneno hayo akiyalaza macho yake, na kumtazama Vivi aliye juu ya kifua chake akijiliza kwa msisimko wa furaha.

"Nakupenda sana Labi." kwa kilio akatamka maneno hayo akiwa kifuani mwa Labi. Ni mbele ya mboni za wazazi wa familia zote mbili zikiwa zinashuhudia. Ilikuwa furaha na fahari mno, vijana wao wakionesha upendo mkubwa wa kihisia, wanaotunziana mioyoni.

"Ila ni vile tu labda haikuandikwa, lakini nilitamani sana na rafiki zangu wawili wangekuwepo hapa saa hii, washuhudie mwanamke niliyempata kwa mchango wao mkubwa, akielekea kuwa wangu wa milele." Hapo huzuni zilipenya nyusoni mwa familia hizo mbili, alipozungumzia kutamani kwake kama Jax na Imraan wasingefariki na kushiriki tukio hilo. Ndiyo hao rafiki zake aliowamaanisha, hakuna ambaye hakujua mahusiano ya vijana hao watatu kwenye familia hizo.
Alihitimisha Labi, sherehe hiyo ikaendelea ndani ya jumba hilo la kifahari, walikuwa wachumba rasmi tayari. Pia siku ya ndoa yao haikuwa mbali, ilipangwa kufanyika wiki moja mbele baada ya tukio hilo la kuvishana pete walilotimiza usiku huo. Hiyo ilikuwa mara ya pili kwa familia hizo mbili kukutana, awali ikiwa ndani ya Hotel

ya Mzee Aloyce Cosmas, baba yake na binti Vivi, ambapo aliialika familia hiyo ya mzee Kimati, ikiwa mwanzo wa ukaribu wa familia hizo mbili, uliojengwa kwa mahusiano ya watoto wao waliopendana. Mzee Aloyce pia alikuwa mtu mwenye uwezo kifedha, japo hakumzidi Kimati Sesewa. Hadithi za furaha hazikuweka tuo, ziliendelea na kutamalaki pahala hapo, huku Familia zikila na kuzungumza pamoja ndani ya jumba hilo limilikiwalo na mzee Kimati Sesewa.

* * *

Tayari kazi ipo mikononi mwake Inspekta Azizi Kasese. Ni jukumu zito la kumsaka kiumbe ama viumbe, maana bado haikujulikana. Kiwiko cha mkono wake kikiwa juu ya meza, baadhi ya viganja vyake chini ya kidevu, huku kidole chake cha shahada kikichezacheza juu ya midomo yake aliyoifunga, vyote hivyo vilifanyika kwa mkono wake wa kushoto akiwa ndani ya ofisi yake akitafakari kwa umakini, ni wapi aanzie. Alishika simu yake na kuanza kuzipitia zile video fupi za mauaji ya Jax na Imraan, hadi na ambazo zilionesha sehemu iliyoachwa miili yao iliyo ndani ya kiroba.

Alitazama kwa kina huku akifafanua jambo na punde akaacha. Ni usiku huohuo uliozikutanisha familia ya Labi na Vivi waliokuwa wakifurahia tukio la uchumba wao. Inspekta Kasese akavuta simu hewani, aliwasiliana na mtu sekunde kadhaa kisha akatua simu yake mezani. Lisaa limoja mbele alionekana kuwa mtaani, ni uswahilini.

"Sikia Domy, kabla ya kufanya mengi, nahitaji unitafutie chochote kuhusu hawa vijana, marafiki zao au watu wenye mahusiano nao ya karibu, lifanyike si juu ya masaa 24 kuanzia sasa."
"Sawa kiongozi." Alimkabidhi picha za marehemu Jax na Imraan kisha wakaagana na kila mmoja kupita njia yake. Inspekta Kasese alirejea kwenye gari yake ndogo na kupotea.


Domy alikuwa kijana anaefanya naye kazi nyingi kwa usiri mkubwa. Kijana tu wa mtaani, mtoto wa mjini anayeishi kijanja mno, suluhisho la matatizo mengi ya haraka ambayo sio halali, na hadi halali pia. Kama unataka hati ya kusafiria pasii kuchelewa muone Domy, cheti cha kuzaliwa, viwanja, nyumba, simu, laptop. Wewe kama unashida hadi ya mwanamke muone Domy. Kwa wengine Domy alitumika hivyo, lakini kwa Azizi Kasese alikuwa na matumizi tofauti, alishamfanya mpelelezi wake katika misheni nyingi alizozitimiza kwa ushindi, leo alimkabidhi kazi ya kufahamu chochote kinachowahusu vijana wawili waliouwawa, tena watoto wa viongozi wazito kabisa katika Taifa.

Domy alilipokea jukumu hilo bila kusita. Pakakucha, ilikuwa kabla ya majira ambayo yaliwakutanisha jana yake, Domy alimtafuta Inspekta Kasese, walikutana tena na kuketi ndani ya gari.
"Kitu pekee nilichokipata ndiyo hicho mkuu, walikuwa vijana wala bata mno, walipenda starehe kama masikio ya msichana yoyote kwa sauti ya mashine ya ATM." aliongea akiwa anakabidhisha simu yake kwa Azizi Kasese iliyo na picha juu ya kioo.
"Lakini pande nyingi walionekana watatu, inasemekana waliongozana sehemu nyingi wakiwa pamoja, na walikuwa marafiki wakubwa mno." aliendelea kutoa maelezo Domy, huku akipangusa kioo cha simu yake iliyo mikononi mwa Azizi, na kutokea picha nyingine. "Huyo ndiyo mtu pekee wa karibu na hao marehemu wawili, anaitwa Labi Kimati, anaishi upanga, baba yake ni bwana Kimati Sesewa, miongoni mwa matajiri wakubwa wa nchi hii."

"Sawa, mfuatilie nini anafanya kwa sasa, na mienendo yake." aliongea na kutoa kibunda cha pesa na kumkabidhi Domy.

Baada ya jukumu la kwanza kulikamilisha, sasa anapewa kazi ya pili, ni kumfuatilia Labi Kimati.

*Itaendelea...*



# RIWAYA: NGUVU YA KIAPO (01)- Na: Eva Mrema

**SURA YA KWANZA**

Nilikutana naye kwenye baa maarufu mkoa ule wenye baridi nyepesi ya kukonga mifupa. Sikuwa mlevi, nilionja mvinyo mwepesi mara chache; ile baridi na utulivu wa nyumbani usiku, havikuivana kabisa. Kilichoniweka mahali pale ni muziki mubashara uliopigwa kila usiku wa alhamisi.

Mara moja moja niliimba. Ndio niliimba na hii hii sauti yangu isiyo vutia. Masikioni kwangu nilijisikia vizuri. Baadhi ya waliochagua kunielewa walipenda namna niliimba. 'Let her go' wimbo wa msanii Passenger. Niliuimba kwa hisia sana, na hata siku aliponiona kwa mara ya kwanza nilikuwa nikiuimba wimbo huo.

Alinitazama kwa huruma, sijui alihisi nini kwenye sauti yangu iliyoanzia ndani kabisa kwenye mizizi ya moyo wangu. Baada ya kuimba nilishuka pale kwenye jukwaa lililonizoea mithili ya uwanja wa nyumbani. Makofi yalipigwa haswaa! Na moyo wangu mnyonge uliitika. Nilivalia taiti nyepesi ya rangi nyeupe iliyozichonga vyema bastola zangu ndogo. Juu nilitinga fulana nyeupe kubwa niliyoikunja kidogo mikononi na kuichomeka kiunoni upande mmoja. Chini nilipiga raba kali niliyoinunua memoria. Nilikuwa msafi na nilivutia sana. Hatua za madoido ya kike, zilinipeleka kwenye meza ndefu iliyokuwa na kiti kimoja. Hii ilikuwa kona yangu niliyoichagua siku zote.

Nililetewa Redbull na maji makubwa ya Kilimanjaro. Nilianza kuchanganya mchanganyiko wangu kwenye glass na kisha kuugigida kinywani kwa uchu. Nilijimwagia kidogo kitu kilichonifanya nishtuke. Nilichukua tishu na kujipangusa. Nilihamaki baada ya kumuona. Alisimama upande wangu wa pili kama kioo kilichonionesha taswira tofauti yenye tabasamu mfanano na langu.

Nilistaajabu, walakini muonekano wake ukamaliza maneno kinywani mwangu. Nilikuwa sipendi kabisa mtu aingilie starehe yangu. Kilichonikokota usiku na kuususa usingizi nilioutafuta kwa tochi, ni muziki na sio kukutana na watu wapya hali ya kuwa wa zamani sikufanikiwa kuwamudu.

Nilimsabahi na kumtoa kwenye bumbuwazi alimojiweka kwa hiyari yake. Alishituka na kunipa mkono tusabahiane. "Hellow!" Ilikuwa salamu aliyoituma kwangu na kunifanya nicheke. Sio kwamba sikuielewa, ni vile nimezoea kuitumia nikipokea au nikipokelewa simu. Nikamwambia hi! Hali tukipeana mikono, ishara ya uungwana.

"My name is Sunche Godwill, will you mind if I ask for your company tonight?" Nilijitoa mkono wangu kwenye mkono wake ulioendelea kunishikilia hata baada ya salamu. Sikujibu chochote mfano wa mtu ambaye hakuielewa lugha. Nilimkagua juu hadi chini, kimo chake futi sita na nukta hamsini. Mguu alionekana kuvaa namba arobaini na tatu kwa makadirio yangu. Mwili wake ulikuwa wa kawaida; sio kibonge tipwa tipwa, wala si mwembamba kama mbao. Alivaa kaptura ya kiume rangi ya zambarau mbivu na shati la mikono mirefu alilolikunja na hakuwa kafunga vifungo vyote. Jambo lililopelekea macho yangu kutazama mgawanyiko wa kifua chake.

Ni mara ya kwanza kuonana mimi na yeye, sikutaka kuendekeza jambo ambalo mwishowe lingenitokea puani. Nilimwambia "unaweza kuniacha nikae mwenyewe?" Sikutarajia kama angenielewa. Aligeuka na kuanza kuondoka. Nilishika kinywaji changu, nikaweka mdomoni na kuanza kunywa. Alirejea kwa ghafla na kuniuliza jina langu. Nilishtuka mno, kinywaji kikanipalia. Nilikohoa mfululizo, hakusita kunikaribia na kutaka kunishusha kwenye kiti kile ila nilikataa. Alitaka tu anisaidie kurejesha hali yangu aliyojilaumu kuwa kitenzi kisababishi.

Alinikaribia zaidi na kunisugua mgongoni taratibu. Niliisikia sauti ya 'pole' iliyojirudia mara kadhaa. Alisisitiza nishuke juu ya ile stuli ndefu. Kwa msaada wake, nikashuka. Alinipatia maji. Niliyanywa na

hapo nikashusha pumzi. Sikutaka kurejea kukaa pale juu tena kama ngongoti. Niliangalia sehemu nyingine ambayo haikuwa na raia.

Niliyaendea makochi yaliyojizunguka yenyewe kutengeneza upekee, mfano wa kajumba kadogo. Niliketi. Bwana Mzungu alinifuata nyuma kama mkia na nilipotaka kumpa onyo nikabaini alinibebea mkoba na vinywaji vyangu nilivyovisahau kwa kitete cha kupaliwa.

“Asante sana” nilipokea vitu na kuketi. Aliitikia kwa kutikisa kichwa kisha akaniuliza hali ameusinyaisha uso wake, “naweza kuketi na wewe? Samahani kama nimekuwa mgumu kuelewa”

Nilitabasamu kisha nikamkubalia kuketi. Alinitazama sana. Baadae nikakumbuka kuhusu swali la awali. “Naitwa Tabita Komba” nilijitambulisha na kumuomba arudie jina lake, kwani sikumzingatia mwanzo.

“Don’t worry naitwa Sunche Godwill. Nimefurahi kukutana nawe Tabita” nilijikaza nisicheke maana jina lake kuna namna likikutana na Kapeto ni vituko. Nilimuuliza anafanya nini katika mji ule; alitabasamu, “Nafanya kazi kama mkufunzi mkuu wa Chuo kikuu cha Kampala hapa nchini” nilitikisa kichwa ishara ya kukubali maelezo yake. Chizi muziki mimi! Ukapigwa wimbo nilioupenda, nilinyanyuka bila hofu wala uoga karibu na mgeni. Nilianza kucheza, kama kuna mtu anaijua ‘coconut tree’ basi ndo ulikuwa wimbo mpya mjini wakati huo. Nilijibanabana, ila nilicheza. Ulipotamatika wimbo niliketi, nilishika maji na chupa lake nikayamimina mdomoni.

Niliposhusha nikabaini jambo.

Bwana Sunche alifurahia sana kunitazama, namaanisha alifurahia sana. Alinitazama hali akitabasamu na kupotelea kabisa kimawazo. Nilimshtua nilipomsaili jambo ambalo hakulisikia kabisa, nililazimika kurudia swali. “Unaishi wapi?

“Naishi Moshono nyuma ya supermarket,” alinijibu. “Unaongea kiswahili kizuri sana, umeishi muda gani Tanzania?” “Miezi kumi na nane. Ubora wangu wa lugha ni kwa sababu niliisomea, napenda Kiswahili, naipenda Tanzania, kuna mara nilijisemea uzee wangu nitaumalizia Tanzania, nikiwa na familia yenye nusu ya asili ya kitanzania” alipiga funda moja kwenye mvinyo wake na kabla hajaendelea akanisihi kubadili kinywaji.

Niliagiza mvinyo mlaini maana kichwa changu hakikutaka kabisa hekaheka usiku huu. “Unafanya nini wewe Tabita? I mean unafanya kazi gani?

“Mimi ni mhasibu kwenye kampuni binafsi” nilimjibu. Muhudumu aliwadia na kunipatia kinywaji changu. Tuliagiza nyama choma na kungoja kwa utulivu hali tukiburudika. “Nimefurahi kukutana na wewe Tabita” “Asante, nimefurahi pia kukutana na Mzungu anayezungumza Kiswahili kizuri namna hii” nilimwambia.

Tulipata dakika za ukimya na kila mmoja kuburudika kwa nafasi yake. Tulikula, tulikunywa, na muda wangu ulipowadia nikaaga kuondoka. Aliambatana na mimi hadi nje ambapo niliendea gari langu na kuingia ndani. Nilifunga milango, kisha mkanda. Nilifungua kioo na kumpungia kama ishara ya kumuaga. Niliondoka eneo lile na kuelekea moja kwa moja nyumbani.

**RIWAYA: NGUVU YA KIAPO**

Inapatikana katika kitabu (nakala ngumu) na soft copy (nakala tepe) kwa bei ya kirafiki.

**KITABU** - Tsh 10,000
**Dar es salaam:**

- Duka la Kona ya Riwaya - 0655428085
- Kalamu Tulivu Magomeni - 0718975659
- Posta Mpya kwa Joji - 0713454152
- Temeke kwa Eva Mrema - 0742630141

Soft Copy (Nakala tepe) PDF - Tsh 5,000
‘Offer’ kupitia Ngurumo ya Mwandishi ni - Tsh 3,000
Lipa kwa **MPESA LIPA NAMBA 36499709 Eva John Mrema**

# Tangazo

*Tangaza nasi kwa tsh 5000 tu*

*Hapa!*


www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi

jamvilasimulizi@gmail.com